Jumamosi Januari 4, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe


ISSN 0856 • Na. 0580119
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US






## Babu miaka 80 atinga kortini tuhuma kubaka mtoto miaka 13

UKURASA 10



# JPM aona fursa mpya za ajira

UKURASA 2



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na wafanyabiashara wa korosho wa mikoa ya Mtwara na Lindi, katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

## Kabendera atuma ujumbe mzito kutoka mahabusu

• **Wasomwa** ibada ya kuaga mwili wa mama yake, waombolezaji wabubujikwa machozi...*Endelea uk.2*

## Kunradhi Vicent Bruno Minja

UKURASA 2

**MICHEZO** **AZAM YAPANIA KUREJEA VITANI** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Kunradhi Vicent Minja

KATIKA toleo letu la Jumamosi Desemba 21, mwaka jana, tulichapisha habari yenye kichwa cha habari 'Wacharuka viongozi wa mtaa kuuza eneo la wazi', iliyoeleza kuhusu baadhi ya wananchi wa Mtaa Ali Hassan Mwinyi, Mikocheni A, jijini Dar es Salaam kufanya maandamano dhidi ya viongozi wao wa mtaa.

Wananchi hao waliandamana kwenda kwenye ofisi za uongozi wa serikali ya mtaa wao wakilalamikia kile walichodai uongozi wa serikali za mitaa katika eneo hilo, umeuza eneo la wazi kwa mwekezaji.

Eneo lililolalamikiwa na wananchi hao ni kiwanja Na. 628 walichodai ni eneo la wazi. Hata hivyo, udadisi wa Nipashe umebaini kiwanja hicho kilikuwa na mgogoro wa muda mrefu, lakini ulimalizwa na Mahakama Kuu (Divisheni ya Ardhi) kupitia hukumu yake ya Februari 24, 2014, ikimtambua Vicent Bruno Minja kuwa anakimiliki kihalali.

Udadisi wa Nipashe ulibaini kuwa hukumu hiyo iliyosomwa na Jaji Mgetta, ilitolewa baada ya miaka minne ya uwapo wa kesi hiyo mahakamani dhidi ya umiliki wa kiwanja hicho.

Nipashe pia imebaini kuwa mwaka 2018, Damas Assesy na Flora Assesy, walifungua jalada Mahakama ya Rufani Tanzania kuzuia kwa muda utekelezaji wa hukumu ya Mahakama Kuu (Ardhi) kuhusu uendelezaji wa kiwanja hicho, lakini maombi yao yalikataliwa na mahakama hiyo ya juu zaidi nchini Aprili 11, mwaka jana.

Kutokana na hali hiyo, Nipashe tunamwomba radhi mmiliki wa kiwanja hicho, Vicent Minja na wasomaji wetu kwa usumbufu uliojitokeza.

**MHARIRI**

# JPM aonyesha fursa za ajira

**Na Mwandishi Maalum**

RAIS John Magufuli ametoa wito kwa Watanzania wengi zaidi kujitokeza kufuga wanyamapori kupitia bustani za wanyama (zoo), ili kuongeza idadi ya wanyama hao na hivyo kupanua fursa za utalii na ajira.

Kiongozi huyo mkuu wa nchi amewapongeza baadhi ya Watanzania walioanzisha 'zoo' hizo akiwamo Luteni Jenerali mstaafu Samwel Ndomba (Lugari Mini Zoo - Mbinga), Dar es Salaam Zoo, Bahari Zoo na wengine ambao wamefuga wanyamapori katika bustani na mashamba yao.

Rais Magufuli alitoa rai hiyo jana alipokuwa anazungumza na maofisa na askari wanyamapori wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) walioko katika Hifadhi ya Taifa ya Kisiwa cha Rubondo.

Alifafanua kuwa ufugaji wa wanyamapori unaruhusiwa kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 na Watanzania wanayo haki ya kuwapata wanyamapori hao kwa mujibu wa sheria na taratibu, kufuga mahali popote panapofaa na patakapowezesha watalii wa ndani na nje ya nchi kutembelea.

"Kuna nchi nyingi ambazo wenzetu wananufaika sana kwa ufugaji huu wa wanyamapori ikiwamo Afrika Kusini, wanapata watalii wengi, watu wao wanapata ajira na wanaowekeza kwenye ufugaji huu, wanapata fedha, sioni sababu kwanini sisi Watanzania tusifuge wanyamapori wakati sheria zinaruhusu kufanya hivyo.

"Changamkieni fursa hii ndugu zangu, wataalamu wa wanyamapori wafundisheni wananchi kufuga wanyamapori na wahamasisheni kufanya hivyo, viongozi wastaafu jitokezeni kuonyesha mfano kama alivyofanya Luteni Jenerali mstaafu Ndomba kule Mbinga, maeneo ya kufuga yapo mengi," alisisitiza.

Rais Magufuli aliongeza kuwa serikali imedhamiria kupanua na kuboresha maeneo ya vivutio vya utalii, akieleza kuwa katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake, hifadhi za taifa zimeongezwa kutoka 16 hadi 22 na nyingine ziko mbioni kuanzishwa, kutokana na kutambua kuwa utalii ni sekta inayochangia vizuri katika pato la Taifa na inatoa ajira kwa Watanzania wengi.

Kwa sasa Tanzania ina zoo 23, mashamba ya wanyama 20 na ranchi sita.

Wizara ya Maliasili na Utalii inabainisha kwamba sekta ya utalii inachangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa, pia ikiipatia nchi asilimia 25 ya fedha zote za kigeni na kutoa ajira za moja kwa moja 600,000 na nyinginezo zaidi ya milioni mbili.

Sekta ya Utalii na Uhifadhi inajumuisha hifadhi za taifa 22 zilizo chini ya Tanapa iliyoanzishwa kisheria mwaka 1959.

Maeneo yake mengine ni Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, yenye ukubwa wa kilomita za mraba 8,292, mapori ya akiba 28, yenye kilomita za mraba 114,782.47 na mapori tengefu 42, yenye ukubwa wa kilomita za mraba 58,565.02.

Tanzania pia ina hifadhi zenye hadhi ya kimataifa zilizowekwa kwenye orodha ya Urithi wa Dunia, ambazo ni: Pori la Akiba Selous; Hifadhi ya Taifa Serengeti; Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (Kinapa); Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara.



Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Prof. Damian Gabagambi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kabendera atuma ujumbe mzito kutoka mahabusu

**Na Moshi Lusonzo**

MWANDISHI wa habari za uchunguzi, Erick Kabendera, ameandika barua kutoka mahabusu, akiwashukuru Watanzania kwa kumsaidia kukamilisha taratibu za mazishi ya mama yake.

Mama wa mwandishi huyo, Verdiana Mujwahuzi, alifariki dunia Desemba 31, mwaka jana, katika Hospitali ya Amana jijini Dar es Salaam.

Mwili wa Verdiana uliagwa jana katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Xavier, Parokia ya Chang'ombe wilayani Temeke jana, waombolezaji wakiongozwa na Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe.

Mbali na Zitto, kulikuwa na viongozi mbalimbali vya vyama vya upinzani, wanadiplomasia na wananchi.

Kabendera ambaye yuko rumande akikabiliwa na mashtaka matatu likiwamo uhujumu uchumi, juzi aliiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, impe ruhusa ya kwenda kuaga mwili wa mama yake na kuuzika, lakini ilishindikana kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi inayomkabili.

Ujumbe wa mwandishi wa habari huyo uliosomwa wakati wa kuaga mwili wa mama yake na Zitto, ukiibua simanzi na vilio kwa ndugu, marafiki na waombolezaji.

Katika barua hiyo, Kabendera alielezea namna anavyohisi uchungu kukosa kumuaga mama yake.

Aliwashukuru Watanzania kwa kumfariji na kumsaidia kumsitiri mama yake huku akisema jambo hilo limempa faraja na kuiona Tanzania yenye upendo kama yeye anavyoipenda iwe.

Zitto, akisoma barua hiyo, alisema: "Kuna mama mmoja tu, anafariki dunia mara moja, msiba mara moja, msiba wa kuondokewa na mama ni mkubwa sana. Hasa anapokuwa anaondoka na umeshindwa kumuaga kama ilivyotokea kwangu.

"Hata hivyo, nimefarijika kwa Watanzania wote walioguswa na msiba huu, bila kujali itikadi zao za kisiasa na kidini na kunisaidia kumsitiri mama yangu.

"Upendo huu umeonyesha nchi ambayo nimeipenda na naipenda kutoka moyoni. Shukrani za dhati ziwafikie watu wote kwa upendo na ushiriki wao wa kufanikisha msiba wa mama yangu," alisema."

Ujumbe huo uliowasilishwa kupitia wakili wake, Jebra Kambole kwa Zitto, kabla ya kusomwa, ilielezwa kuwa Kabendera alitumia muda mrefu kuandika waraka huo wenye kurasa 20.

Katika hatua nyingine, wanaharakati wa haki za binadamu, walitoa salamu za rambirambi huku wakisema wataendelea kumsaidia Kabendera kisheria na kisaikolojia.

Wanaharakati hao walisema wako pamoja na Kabendera katika magumu anayoyapitia yakiwamo kuondokewa na mama yake kipenzi pamoja na kesi inayomkabili.

HABARI KITAIFA

# Raia Uingereza akiri uhujumu, ahukumiwa

**Na Hellen Mwango**

RAIA wa Uingereza, Jean Banton (22), amehukumiwa kulipa faini ya Sh. milioni 10 au kwenda jela miaka mitatu baada ya kumtia hatiani kwa mashtaka mawili, likiwamo la kusafirisha madini aina ya dhahabu yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 29 bila kuwa na leseni.

Mbali na adhabu hiyo, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imeamuru madini hayo yataifishwe ili kuwa mali ya serikali.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Alisema hukumu hiyo imezingatia mshtakiwa amekiri tuhuma zake mwenyewe na mahakama yake imezingatia kwamba mshtakiwa huyo ni mkosaji wa mara ya kwanza na hakuisumbua.

"Kwa sababu mshtakiwa amekiri makosa yake mwenyewe, mahakama yangu imezingatia asili ya kesi hii, mshtakiwa utalipa faini ya Sh. milioni tano kwa kila kosa na ukishindwa utatumikia kifungo cha miaka mitatu jela," alisema.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon alidai hawana kumbukumbu ya makosa ya nyuma ya mshtakiwa na kuomba mahakama impe adhabu kali iwe fundisho kwake na kwa wengine ambao wana mpango wa kufanya makosa hayo.

Alidai mshtakiwa huyo aliingia nchini kwa lengo la kufanya utalii na siyo biashara ya madini na kwamba hana kibali cha kumruhusu kusafirisha madini hivyo, kitendo alichofanya kinalenga kudidimiza uchumi wa nchi.

Pia, aliomba mahakama kutaifisha madini hayo na kuwa mali ya serikali.

Wakili wa Utetezi, Hamza

INAENDELEA UK. 8



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni (wa tatu kulia), akitoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Idara ya Uzalishaji Vitambulisho, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Alphonce Malibiche, wakati wa ziara ya Naibu Waziri kutembelea kituo cha kanzidata kilichopo Kibaha mkoani Pwani. Wa tatu kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Dk. Anold Kihaule. **PICHA: MAMBO YA NDANI**

# Chadema yakosoa bil. 600/- ujenzi daraja refu Mwanza

**Na Mwandishi Wetu,** ILEMELA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimeukosoa uamuzi wa serikali wa kujenga daraja la Kigongo-Busisi lenye urefu wa Km 3.2 litakalogharimu Sh. bilioni 699.2, kikidai fedha hizo zilipaswa kuelekezwa kwenye miradi inayowagusa wananchi moja kwa moja.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Victoria, Ezekia Wenje, alipozungumza na waandishi wa habari katika ofisi ya kanda hiyo wilayani Ilemela, akidai ujenzi wa daraja hilo si kipaumbele cha wananchi wa kanda hiyo.

Alidai hitaji la wananchi wa Kanda ya Ziwa ni majisafi, huduma za afya, madarasa, nyumba za walimu na chuo kikuu cha serikali.

"Leo tunajengewa daraja na zaidi ya Sh. bilioni 600 zinatumika Busisi - Kigongo, sasa tuulizane watu wa kanda, hivi kipaumbele cha wananchi wa Kanda ya Ziwa ni daraja la Busisi? Hivi ndiyo vipaumbele?" Wenje alihoji.

Mbunge huyo wa zamani wa Nyamagana, alidai upatikanaji wa maji kwa taifa bado unatia shaka, akishuhudia kundi la kinamama wanaofua nguo kandokando ya barabara wakitumia maji ya mvua inayoendelea kunyesha nchini. "Leo (jana) nimetoka Mkoa wa Mara asubuhi, mvua imenyesha, ukifika sehemu inaitwa Buturi, Bunda mpaka maeneo ya Magu, mvua imenyesha sana, kuna chemchemu wanawake wanafua nguo kandokando ya barabara kwenye zile chemchemu. "Maana yake ni kwamba, maeneo wanayopata maji kipindi cha kiangazi ni mbali sana na ndiyo maana mvua inaponyesha, mtu anaenda kufua nguo zake pale, maana yake ni kwamba upatikanaji wa majisafi na salama katika taifa letu bado una mashaka makubwa.

"Hivi kweli Baraza la Mawaziri linakaa na kumshauri Rais kwamba kipaumbele cha wananchi wa Kanda ya Ziwa ni daraja? Wangetumia hiyo 'sixth hundred billion' (bilioni 600), yaani inakimbilia trilioni, hiyo fedha tungepewa hapa Kanda ya Ziwa, hatuna hata chuo kikuu kimoja cha serikali.

"Tungepewa hiyo fedha, tukakamilisha madarasa, tukakamilisha nyumba za walimu, ili watoto wetu na walimu wapate nyumba, tukaimarisha hali ya sekta ya afya, tungepewa fedha hiyo Kanda ya Ziwa tukaambiwa hakikisheni mnamaliza masuala ya majisafi na salama, hivi tungefanya kwa kiasi gani? Wenje alihoji.

Kiongozi huyo wa chma hicho kikuu cha upinzani nchini, alidai anaiona serikali inaamini katika kile alichokiita maendeleo ya vitu badala ya kuamini katika maendeleo ya watu.

# Walia bei kubwa nyama ya ng'ombe

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

BAADHI ya wananchi katika mji wa Tunduru mkoani Ruvuma, wamelia kupanda ghafla kwa bei ya nyama ya ng'ombe tangu kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Kutokana na kupanda huko kwa bei ya nyama, wananchi hao wameiomba serikali kuingilia kati ili kuwafanya wananchi kupata unafuu wa bei na kumudu kuipata bila matatizo.

Walisema wafanyabiashara wanaomiliki maduka ya kuuzia nyama, wamekuwa wakiwaza kitoweo hicho kwa Sh. 8,000 kwa kilo, bei ambayo ni kubwa kulinganisha na maeneo ya jirani, ikiwamo makao makuu ya mkoa, Songea, ambako inauzwa kati ya Sh. 5,000 na Sh. 6,000.

Mwajuma Hamisi na Japhet Mnyagala, ni miongoni mwa wananchi waliotoa kilio hicho mbele ya mwandishi wa habari hii na kwamba awali bei hiyo ilionekana ya kawaida, lakini hata baada ya miundombinu ya barabara kufunguka, bado inaendelea kuwa juu.

"Wakati barabara ikiwa ya vumbi, tuliona hali hiyo kuwa ni ya kawaida, lakini hivi sasa barabara ya lami imekwishajengwa na kuwapunguzia usumbufu wa kuingiza mifugo kutoka maeneo mbalimbali ya nchi. Pamoja na ubora wa barabara bei bado iko juu," alisema Mnyagala na kuongeza kuwa hali hiyo inawafanya wananchi wasione manufaa ya maendeleo hayo.

Baadhi ya wafanyabiashara wanaomiliki maduka ya nyama, Salama Anosisye na Caeser Nyamka, walisema hali hiyo inasababishwa serikali kuwazuia kuingiza ng'ombe wa kuchinja kutoka nje ya wilaya hiyo.

Walisema kutokana na wafanyabiashara hiyo kuongezeka huku wakiwa wanashindana na wafanyabiashara wa maduka ya nyama kutoka Wilaya za Masasi, Nanyumbu, Nachingwea na Newala kutegemea ng'ombe wanaouzwa katika mnada mmoja ulioko Kata ya Muhuwesi, Tunduru, ng'ombe hununuliwa kwa bei kubwa ambayo huwafanya washindwe kuuza nyama kwa Sh. 8,000.

Walisema Wilaya ya Tunduru ina wafugaji wachache ambao wamesambaa katika tarafa za Matemanga, Lukumbule, Nalasi, Namasakata, lakini wamekuwa wakishindwa kupeleka mifugo yao katika mnada mmoja ambao uko Nakapanya.

Kwa mujibu wa wafanyabiashara hao, kikwazo kingine ni kuwapo kwa zuio la wafanyabiashara kununua ng'ombe nje ya eneo la mnada hali ambayo pia imekuwa ikiwapa mazingira magumu ya kuwahudumia wananchi kupata kitoweo chenye unafuu wa bei.

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo na kwamba tayari ameanza kuifanyia kazi kwa kuwaita wafanyabiashara kuzungumza nao kwa lengo la kutafuta suluhu ya kudumu.

# RC wa zamani amfagilia Magufuli

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

ALIYEWAHI kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, John Mwakipesile, ameeleza kufurahishwa na mwenendo wa utumbuaji unaofanywa na Rais John Magufuli ndani ya serikali kutokana na baadhi ya watumishi kuwaza kuiba fedha za umma.

Mwakipesile alisema hayo jana mjini hapa alipozungumza na waandishi wa habari, huku akisema anaridhishwa na kasi ya utendaji kazi wa serikali ya awamu ya tano na kuwa kuna wakati anatamani angefanya kazi na serikali hiyo.

Alisema jambo lingine analompongeza Rais Magufuli ni hatua ya kuimarisha nidhamu kazini kwa kuwa imesaidia jamii kuheshimiana na kuthaminiana miongoni mwa Watanzania.

Kwa mujibu wa Mwakipesile, anamfahamu Rais Magufuli tangu alipokuwa Naibu Waziri wa Ujenzi mwaka 1995 walipoingia wote kama wabunge kwa mara ya kwanza kuwa ni mtu ambaye anachukia uzembe, wizi na ubadhirifu wa mali za umma.

Mwakipesile alisema hata yeye alipokuwa mkuu wa mkoa, aliwahi kumtimua kazini mhandisi wa ujenzi kutokana na ubadhirifu wa mali za umma.

"Unajua hata mimi nikiwa mkuu wa mkoa niliwahi kumtimua mhandisi wa ujenzi kutokana na wizi bila kujali visheria vingi vya haki za wafanyakazi, ndiyo maana nasema ninatamani sana ningefanya kazi na serikali hii ya awamu ya tano," alisema Mwakipesile.

Alisema serikali ya awamu ya tano imefanya kazi nzuri na zinazoonekana ndani ya miaka minne na kuwa kuna umuhimu wa watendaji wa serikali na wananchi kuendelea kumuunga mkono Rais Magufuli.

Hatua ya Rais Magufuli kuimarisha nidhamu kazini, alisema imesaidia kudhibiti mambo mengi yasiyo na msingi ambayo yamekuwa yakifanywa na baadhi ya wafanyakazi maeneo ya kazini.

Mwakipesile alisema kuwa ni wakati wa Watanzania hususani vijana wenye uwezo ndani ya serikali, kumsaidia Rais kufanikisha malengo aliyojiwekea katika utawala wake.

# Kesi vigogo Acacia yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

KESI inayomkabili aliyekuwa Rais wa Migodi ya Pangea, North Mara, Exploration na Bulyanhulu, Deogratius Mwanyika na wenzake, imepigwa kalenda mpaka Januari 17, mwaka huu, itakapotajwa tena baada ya Upande wa Jamhuri kudai upelelezi wake bado haujakamilika.

Mwanyika na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 39, yakiwamo ya kutakatisha fedha na kukwepa kodi ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 112.

Jana, kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Godfrey Isaya, wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Simon Wankyo, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake bado haujakamilika.

Hakimu Isaya alisema kwa kuwa kesi hiyo upelelezi wake bado haujakamilika, washtakiwa wapelekwe mahabusu mpaka Januari 17, mwaka huu itakapotajwa tena.

Mbali na Mwanyika, washtakiwa wengine ni Meneja Uhusiano wa Mgodi wa Bulyanhulu Alex Lugendo, Mkurugenzi Mtendaji wa Pongea, North Mara na Bulyanhuku, Assa Mwaipopo, Kampuni ya Mgodi ya Pangea, North Mara, Exploration na Bulyanhulu.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo kwa mara ya kwanza Oktoba 17, 2018.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka matatu ya kula njama, mashtaka saba ya kughushi, mashtaka 17 ya utakatishaji wa fedha, kuwasilisha nyaraka za uongo kwa Mamlaka ya Mapato (TRA), shtaka moja la kuongoza uhalifu, mashtaka manane ya kukwepa kodi na shtaka moja la kutoa rushwa.

Washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Aprili 11, 2008 na Juni 30,2007 katika sehemu tofauti za Jiji la Dar es Salaam, Kahama mkoani Shinyanga, Tarime Mara, Biharamulo Kagera, maeneo ambayo yapo katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Maeneo mengine ambayo washtakiwa wanadaiwa kutenda makosa hayo ni katika Mji wa

INAENDDELEA UK. 8



Katibu wa Chama cha Walimu nchini (CWT), wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Mwalimu Nazama Tarimo akizungumza Mji mdogo wa Mirerani kuhusu changamoto ya eneo kubwa la Simanjiro juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Lori lingine la mafuta lalipuka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

LORI la mafuta, mali ya Kampuni ya World Oil ya jijini Dar es Salaam, lililokuwa linasafirisha mafuta ya petroli kutoka Dar es Salaam kwenda Zambia, limeteketea kwa moto na kujeruhi watu wawili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alidai jana kuwa ajali hiyo ilitokea juzi saa 10:30 jioni katika eneo la Meta-Igurusi wilayani Mbarali katika Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam).

Alilitaja gari lililoteketea kuwa ni aina ya Scania Tanker lenye namba za usajili T 956 DRT na tela namba T 886 DRV ambalo lilikuwa linaendeshwa na Issa Yusuph (35), mkazi wa Jiji la Dar es Salaam.

Kamanda Matei aliwataja waliojeruhiwa kwenye ajali hiyo kuwa ni Julius Daud (30) na Stanford Mwakyusa (45), wote wakazi wa Kata ya Igurusi wilayani Mbarali ambao waliendа kwa ajili ya kusaidia kuhamisha mafuta kutoka kwenye gari hilo baada ya kuharibika.

Alidai kuwa awali gari hilo liliharibika katika eneo hilo Januari Mosi, mwaka huu na baada ya matengenezo kushindikana, waliamua kuhamishia mafuta kwenye gari lingine lenye namba za usajili T 844 AWJ.

"Waliojeruhiwa ndiyo waliokuwa wanafanya kazi ya kuhamisha mafuta kwenye gari hiyo kwa kutumia mashine ya kusukuma maji (water pump). Sasa, wakati wanaendelea na kazi ulitokea mlipuko kwenye hiyo mashine na kusababisha moto mkubwa ambao uliteketeza gari hilo na kuwajeruhi," alidai.

Kamanda Matei alidai kuwa mbali na gari hiyo kuteketea, pia kulitokea uharibifu kwenye magari mawili ambayo mafuta yalikuwa yanahamishiwa pamoja na gari la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mbeya lenye namba za usajiri SM 4633 ambalo lilikuwa linatumika kuzima moto huo.

Kamanda Matei alisema majeruhi wa ajali hiyo waliwahishwa katika Kituo cha Afya cha Kata ya Igurusi kwa ajili ya matibabu kutokana na majeraha waliyoyapata kwenye ajali hiyo.

Aliwataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuepuka kusogea kwenye maeneo ambayo wanaona kuna hatari ya mafuta kulipuka kwa maelezo kuwa ajali za aina hiyo zinakuwa na madhara makubwa.

Mwaka jana, ajali ya moto ilitokea katika eneo la Msamvu Itigi mkoani Morogoro wakati wananchi walipokuwa wanachota mafuta yaliyokuwa yanamwagika baada ya lori la mafuta kuanguka. Zaidi ya watu 100 walifariki dunia katika ajali hiyo na kuwa miongoni mwa matukio ya hatari zaidi kuwahi kutokea mwaka 2019.



Gari aina ya Hiace yenye namba za usajili T 836 DEB ikiwa imeangukia ndani ya mtaro wa barabara, katika eneo la Ushirika Shinyanga Mjini, baada ya kupata ajali na kujeruhi watu 10. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Likizo yakwamisha kesi ya Zitto Kabwe

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imeshindwa kuendelea kusikiliza kesi ya uchochezi inayomkabili Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, baada ya hakimu anayeisikiliza kwenda likizo.

Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa hoja za pande zote mbili za kama mshtakiwa ana kesi ya kujibu au la.

Hata hivyo, kwa kuwa Hakimu Huruma Shaidi, anayesikiliza kesi hiyo yuko likizo, Hakimu Chaungu alisema itaendelea kusikilizwa Januari 10, mwaka huu.

Awali mahakamani hapo, Upande wa Jamhuri uliita mashahidi 14 kuthibitisha makosa ya uchochezi dhidi ya Zitto.

Katika kesi hiyo, Zitto ambaye ni Mbunge wa Kigoma Mjini, anakabiliwa na mashtaka matatu ya uchochezi, akidaiwa kutenda makosa hayo Oktoba 28, 2018 katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika katika ofisi za makao makuu ya ACT-Wazalendo.

# Kasi ukataji miti bado yatisha

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

KASI ya ukataji misitu nchini bado inatisha, ikielezwa kuwa kwa mwaka, zaidi ya hekta 470,000 za misitu zinakatwa huku mikoa ya Kanda ya Ziwa ikichangia kwa asilimia 17 uharibifu huo.

Imeelezwa kuwa shughuli za kibinadamu ukiwamo uchimbaji madini, zinaongoza kwa kuchangia hali hiyo na kwamba ifikapo mwaka 2025, kiwango cha uharibifu kitaongezeka maradufu iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasu, aliyasema hayo jana wakati akikabidhi mizinga 200 yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 16 kwa vikundi 10 vya wajasiriamali wafugaji nyuki katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

Alisema hali ya ukataji miti havivumuliki na ni lazima hatua za makusudi zichukuliwe kukomesha hali hiyo vinginevyo itakuwa ni kukaribisha maafa.

"Kasi hiyo inatisha sana kwani bila kuchukua hatua madhubuti kuidhibiti, ifikapo mwaka 2025, kasi inaweza kufikia hekta 500,000, hii haikubariki na serikali imejipanga, iko kazini kuhakikisha kasi hiyo inakomeshwa kwa kutumia vikosi vyetu vilivyopewa mafunzo maalum na kuangalia utaratibu mpya wa utendaji kazi katika ya maofisa walioko chini ya Tamisemi na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuongeza ufanisi," alisema.

Kanyasu alisema matokeo ya hatua za kuchukuliwa kutokana na mapendekezo ya mawaziri wanane wa wizara zilizoshiriki kufanya tathimini ya uhitaji wa maeneo zaidi kwa wananchi na hifadhi za misitu iliyoathiriwa na shughuli za kibinadamu nchini mwaka jana, yatatolewa kuanzia mwezi huu.

Katika hafla hiyo, Kanyasu alikabidhi vikundi 10 vya wafugaji nyuki mizinga 200 yenye thamani ya Sh. milioni 16, Ofisi ya Wakala wa Huduma ya Misitu Wilaya ya Geita, ikibainisha kuwa vikundi 26 vyenye wanachama 336 vya ujasiriamali wafugaji nyuki wilayani Geita vimezalisha kilo 6,937.2 za asali katika kipindi cha mwaka jana na sasa vina mizinga ya kisasa 5,405.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MNADA WA FORODHA KWA NJIA YA MTANDAO

**Dar es Salaam, Januari 2, 2020:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wananchi wote kuwa, kwa mara ya kwanza, mnada wa forodha kwa njia ya mtandao utafanyika tarehe 2 hadi 6 Januari, 2020 kupitia Tovuti ya TRA ambayo ni www.tra.go.tz.

Mnada huo utaanza saa 6:00 usiku tarehe 2 na kumalizika saa 5:59 usiku tarehe 6 Januari, 2020 ambapo washindi watatangazwa tarehe 7 Januari, 2020 kupitia tovuti ya TRA.

Ili kushiriki mnada huo kwa njia ya mtandao, mwananchi anatakiwa: -

1. Awe na kifaa kilichounganishwa na mtandao, kama vile Simu ya mkononi, Kompyuta ya mezani, Kompyuta mpakato yaani laptop n.k;
2. Awe na Namba ya Utambulisho ya Mlipakodi yaani TIN na kama hana TIN atatakiwa kujisajili kupitia tovuti ya TRA ya **www.tra.go.tz** ili kupata TIN kwanza;
3. Awe na barua pepe yaani ***email address;***
4. Awe na namba ya simu;
5. Awe amejisajili kwenye tovuti ya TRA kupitia ukurasa wa mnada kwa kubonyeza sehemu ya juu iliyoandikwa ***Auctions;***
6. Wakati wa kujisajili, mshiriki atahitajika kuhakiki kama jina alilojisajili limeshatumika na mtu mwingine ama la kwa kubonyeza kitufe cha tafuta **(Search icon)**. Hata hivyo, mtu yeyote anaweza kuona bidhaa zilizotangazwa kupitia mtandao hata kama hajajisajili;
7. Baada ya kujisajili, mshiriki ataweza kushindana na washiriki wengine kwa kuweka bei na atakuwa na uwezo wa kuongeza bei kadri ushindani utakavyokuwa ukiendelea;
8. Mshindi atapata ankara ya malipo ya awali ya asilimia 25 na ankara ya malipo ya kumalizia ya asilimia 75 kupitia mtandao na atakwenda benki kwa ajili ya kulipia;
9. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia 25 mara baada ya kupata ankara ya malipo wakati ankara nyingine ya malipo ya asilimia 75 atatakiwa kulipia ndani ya saa 48 ingawa kwa chombo cha moto kama vile gari, pikipiki n.k kutakuwa na ankara nyingine kwa ajili ya kulipia ada ya usajili; na
10. Baada ya kukamilisha malipo, mshindi atatakiwa kufika eneo la forodha mzigo ulipo kwa ajili ya kuchukua mzigo wake akiwa na uthibitisho wa kuonyesha kuwa yeye ndiye mnunuzi halali.

Kupitia taarifa hii, wananchi wote walioko ndani na nje ya nchi wanakaribishwa kushiriki mnada huo wa forodha kwa njia ya mtandao wenye haki sawa kwa kila mtu atakayeshiriki mnada.

Kwa maelezo zaidi, mwananchi anaweza kupiga simu katika Kituo cha Huduma kwa Mlipakodi kwa namba za bure **0800 75 00 75 au 0800 78 00 78.** Pia, anaweza kutuma ujumbe kwa njia ya WhatsApp namba **0744 23 33 33** au kutuma barua pepe kwenda: **huduma@tra.go.tz.**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**

**Richard Kayombo**
**Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi**

215571902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viwango klabu za Ligi Kuu viimarishwe kuibeba Stars

**WAKATI** timu ya soka ya Taifa (Taifa Stars) ikiwa imetinga hatua ya makundi ya kuwania tiketi ya kushiriki katika fainali zijazo za Kombe la Dunia, na kikosi chake cha wachezaji wa ndani kikifuzu kucheza michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (CHAN), maandalizi ya timu hizi yanaanzia kwenye Ligi Kuu Bara.

Taifa Stars ambayo sasa inafundishwa na Kocha Mkuu, Etienne Ndayiragije, ilitinga hatua ya makundi baada ya kuwaondoa Burundi, huku timu yake inayokwenda katika fainali za CHAN ilipata tiketi hiyo kufuatia ushindi wa jumla wa mabao 3-2 dhidi ya Sudan.

Kufuzu ilikuwa ni jambo moja, ambalo ni kubwa na la kujivunia kwa Watanzania wote, lakini kinachotakiwa kufanyika sasa ni kuwapo kwa maandalizi sahihi ya timu hizo.

Ili Tanzania iende katika mashindano hayo mawili yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ikiwa imara, ni lazima kuwapo na Ligi Kuu Bara yenye ushindani na inayochezwa kwa kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa.

Kwa nini tunasema haya? Kwa sababu idadi kubwa ya wachezaji wanaounda Taifa Stars wanatoka kwenye Ligi Kuu Bara, ambayo mzunguko wake wa kwanza unatarajia kukamilika wiki hii kwa timu kushuka kwenye viwanja mbalimbali.

Ni wazi kuwa, Ligi Kuu Tanzania inapokuwa yenye ushindani, wachezaji wake watakuwa imara na wenye viwango vizuri ambavyo vitakuwa tayari kushindana na nyota wa mataifa mengine.

Ni wazi kuwa hata kwenye fainali zilizopita za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2019), zilizochezwa mwaka jana, Taifa Stars ilikuwa ndio timu pekee yenye wachezaji wengi wanaocheza nyumbani, wakati Senegal ambayo walipangwa kundi moja, haikuwa na nyota hata mmoja anayecheza kwenye ardhi ya nyumbani.

Kama ni hivyo, klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, zinatakiwa kujiandaa vema kuanzia katika mchakato wa usajili na maandalizi ya vikosi vyao, kwa faida ya taifa.

Umefika wakati wadau wa soka kila mmoja akaamini kuwa maandalizi ya kikosi cha Taifa Stars yanatakiwa kuanzia kwenye ngazi ya klabu na kamwe si ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), peke yake.

Ukiondoa timu hiyo, kikosi kilichobakia ambacho kitakwenda kupeperusha bendera ya nchi katika fainali za CHAN zinazotarajiwa kufanyika Aprili huko Cameroon, ndio haswa kinahitaji kuona ushindani katika Ligi Kuu Bara unaongezeka kwa sababu hali hiyo itasaidia kuimarisha na kuwajenga wachezaji.

Kambwe ligi nyepesi, isiyo na ushindani au isiyofuata kanuni na taratibu, haiwezi kutumika kuwaandaa wachezaji na michuano hiyo mikubwa ambayo itawapeleka kukutana na nyota wanaocheza ligi zilizoendelea kama Algeria, Morocco na Misri.

TFF inatakiwa kusimama imara kuhakikisha hakuna timu inayovunja kanuni kwa sababu kwa kufanya hivyo, haitasaidia kuimarisha wachezaji ambao taifa linawategemea.

Nipashe linawakumbusha pia wachezaji binafsi kuendelea kujituma wakapokuwa katika klabu zao na vile vile kujiandalia programu binafsi, ambazo tunaamini zitawasaidia kuwaimarisha na kuwa tayari kukabiliana na ushindani katika michuano wanayokwenda kushiriki mwaka huu.

Mafanikio katika soka hayapatikani kwa miujiza, hayapatikani kwa njia ya mkato, kinachotakiwa nchi kushiriki katika maandalizi sahihi yanayowaweka wachezaji tayari kwenda kupeperusha vema bendera ya Tanzania katika michuano hiyo.

Maandalizi ya zimamoto hayatakiwi kuwapo katika dunia hii, klabu ndio zinakaa muda mrefu na wachezaji na ndio zinawamiliki, hivyo wanatakiwa kuwaweka wachezaji katika hali nzuri na kutekeleza programu za makocha wao kikamilifu, ili pale watakapofika kwenye kambi ya Taifa Stars, wawe kwenye kiwango bora na chenye kusaidia kusaka matokeo chanya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Nani ataibuka na ushindi leo?

Na Barnabas Maro

**"LIANDIKWALO** ndilo liwalo." Jambo lililoandikwa na Mungu ndilo linalokuwa. Yaani jambo ajaliwalo mtu ndilo limjialo, liwe baya au zuri.

Tunaambiwa "Kinywa ni jumba la maneno." Maana yake kinywa cha binadamu ni kama jumba la maneno. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kuwa binadamu ana uwezo wa kusema maneno yoyote yawe mazuri au mabaya.

"Hauchi hauchi unakucha." Mtu husema usiku hauchi, hauchi, lakini hatimaye jua huchomoza na usiku ukatoweka. Methali hii hutumiwa kumtia mtu moyo anapokabiliana na hali ngumu kumshajiisha* kuwa lazima atauona mwisho wa hali hiyo.

*Shajiisha ni kitendo cha mtu kumhamasisha mwingine kuwa na ari ya kufanya jambo. 'Shajiika' ni kitendo cha mtu kuingia hamu ya kufanya jambo; hamasika. Simba na Yanga kila moja ina hamu ya kuishinda nyingine; si leo tu, bali kila zikutanapo. Timu hizi zaweza kushindwa na timu zingine zote hata za madaraja ya chini lakini hazisononeshwi (kitendo cha kusababisha kuwa na huzuni kubwa moyoni) sana, endapo mojawapo ikishindwa na nyingine!

'Watani' ni watu aghalabu (kwa kawaida; mara nyingi) wa kabila tofauti au rafiki mkubwa ambaye ameruhusiwa kumdhihaki mwingine kwa mujibu wa mila zao bila ya aliyetaniwa kukasirika. Eti Simba na Yanga zaitwa "watani wa jadi." Watani ni watu wanaosaidiana wakati wa dhiki (usumbufu unaosababishwa na matatizo; shida, mashaka). Kwa hali hiyo husaidiana kumaliza matatizo yao.

Kwa Simba na Yanga, 'utani' umegeuzwa kuwa 'chuki' (hisia ya kutopenda kitu au jambo) kwani ni wachache sana wa pande zote mbili wanaokubali kushindwa ilhali robo tatu ya wanachama na mashabiki wao hawakubali kushindwa! Hawajui maana ya ushindani kuwa kuna kushinda na kushindwa!

Kama Simba na Yanga ni 'watani wa jadi' wanaoishi jiji moja liitwalo Bandari ya Salama ambalo ndiyo Dar es Salaam ya sasa, kwa nini ziwekeane shonde (hali ya watu kutozungumza pamoja) ilhali wote ni wa aina moja na sampuli moja?

Yashangaza kusikia eti timu hizi zilikuwa moja zilipoanzishwa mwaka 1935 kabla ya kufarakana mwaka uliofuatia (1936) na kuundwa Sunderland enzi zile ambayo sasa ndio yaitwa Simba SC au 'Wekundu wa Msimbazi.'

Eti sasa timu hizo zaitwa 'watani wa jadi' ilhali zaombeana mabaya kila uchao! Ni utani wa aina gani kumbe zachukiana kama walivyo Waarabu na Waisraeli? Timu yoyote ngeni inayokuja Tanzania kucheza na hizi kongwe ziitwazo 'watani wa jadi' hushangiliwa na 'mtani wa jadi' aliye nnje ya uwanja. Mwenzao akipigwa na mgeni, 'mtani wa jadi' hushangilia utadhani mwenyeji ndiye aliyeshinda.

Mbona twajidharaulisha kiasi hiki hata twaonekana majuha (watu wenye uwezo mdogo wa kufikiri au kuelewa mambo; wapumbavu, wajinga, mabwege)?

Nduguyo anapigwa na mgeni wewe washangilia kipigo chake? Nchi yako yavamiwa na kushambuliwa na maadui wewe wapiga ngoma kuwapongeza wavamizi wanavyoshambulia na kuisambaratisha nchi yako? Kwa hali yoyote iwayo, unapaswa kupimwa akili yako. Tutoke huko turudi kwenye mechi ya leo kati ya Simba wakiwa wenyeji na Yanga wakiwa wageni kwenye mzunguko huu wa kwanza wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara. Hapana shaka kuna mengi waliyoambiwa wachezaji wa timu zote mbili ikiwamo kuahidiwa zawadi za fedha, vyombo vya moto n.k. kwa timu itakayoshinda. Ahadi hizi ni hatari kwa timu kwani wachezaji wasiotumia akili hucheza bila kufuata kanuni za mchezo. Ahadi hizo husababisha wachezaji wasio na hekima kucheza rafu mara kwa mara. Matokeo yake ni kuonyeshwa kadi za njano au kutolewa nnje ya uwanja kwa kuonyeshwa kadi nyekundu. Inapokuwa hivyo, wanaotolewa hukosa michezo mitatu na hivyo kudhoofisha uwezo wa timu husika.

Mwamuzi na wasaidizi wake (washika vibendera) wanapaswa kuchezesha kwa haki bila upendeleo kwani kufanya hivyo ni hatua moja mbele itakayowafanya wachaguliwe kuchezesha mechi za kimataifa.

Idadi kubwa ya watu wanaopenda mchezo wa kandanda wana timu wanazozipenda. Kwa hali hiyo waamuzi wanapaswa kuwa makini na kuchezesha kwa haki hata kama timu wazipendazo zikifungwa na wapinzani wao.

Watambue kwenye mashindano ya kandanda kuna mambo matatu au manne: kushinda, sare (kufungana idadi sawa ya mabao), suluhu (kutofungana) au kushindwa (kufungwa idadi yoyote ya mabao).

Mashabiki nao wanapaswa kutambua kuwa huo ni mchezo, yaani jambo linalofanywa kwa nia ya kuburudisha badala ya kuchukizana, kutukanana na mwishowe kupigana! Kwa nini tugombee gozi la ng'ombe ilhali hatujui nyama kala nani?

Hebu (tamko la kumtaka mtu akusikilize) kwa mara ya kwanza tuoneshe uungwana (hali ya kuwa tayari kumfanyia mtu wema na insafu; utu) ili iwe fundisho kwa wenzetu walio mikoani.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Kortini kwa tuhuma kujeruhi kwa panga

**Na Joctan Ngelly, UJIJI**

MKAZI wa Gungu, Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Joseph Richard (25), maarufu Tereza, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na mashtaka ya kumshambulia Mwamini Hussein na kumkata na panga kichwani na mguu wa kushoto.

Mshtakiwa huyo alifikishwa katika Mahakamani ya Wilaya jana na kusomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi, Eva Mushi, na aliposomewa shtaka lake, alikana kuhusika na kosa hilo, lakini yuko alipelekwa mahabusu kutokana na kukosa mdhamini.

Hakimu Mushi aliyataja masharti ya dhamana kwamba, mshtakiwa kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni mbili.

Upande wa Mashtaka, ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Raymond Kimbe, uldai mahakamani hapo kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa kwa kesi hiyo kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mushi alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Januari 7, mwaka huu kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili Kimbe alidai mahakamani hapo kuwa Agosti 8 mwaka jana, majira ya usiku, eneo la Muongwe, Mkoa wa Kigoma, mshtakiwa alimshambulia Mwamini Hussein kwa kumkata kwa panga sehemu za kichwani na kwenye mguu wa kushoto karibu na goti na kumsababishia majeraha mwilini mwake, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

# Hatarini kukumbwa magonjwa ya mlipuko

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WANANCHI wa Mji wa Tunduru wako katika hatari ya kukumbwa na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu na homa ya matumbo endapo juhudi za ziada hazitachukuliwa kuondoa uchafu uliosambaa katika maeneo mbalimbali ya mji huo.

Haya yamebainishwa na baadhi ya wananchi wa mji huo na kwamba hali hiyo imetokana na kushindwa kuzolewa kwa wakati takataka na kusababisha uchafu kurundikana kwa muda mrefu.

Ally Kufa, Amina Rashidi na Hawa Damla, miongoni mwa wananchi waliopaza sauti zao, walisema juzi kuwa endapo uchafu huo utaachwa uendelee kutamalaki, kuna hatari ya wananchi kuathiriwa na magonjwa ya mlipuko.

Walisema hali hiyo pia inahatarisha afya za watoto wao ambao mara nyingi hucheza katika maeneo ya vizimba vilivyorundikwa taka hizo kwa kipindi kirefu.

Kwa mujibu wa wananchi hao, hali inakuwa mbaya zaidi hasa kipindi hiki cha mvua ambacho maji machafu ambayo hutoa harufu kali hutiririka hadi kwenye makazi ya watu na maeneo ya biashara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Gaspar Balyomi, pmoja na kukiri kuwapo kwa hali hiyo ya uchafu, alisema changamoto hiyo imeanza kushughulikiwa.

Alisema kwa kuanzia kuzoa takataka zilizoko katika vizimba mbalimbali vilivyopo mjini hapa na baadaye watahamia kuzoa taka katika maeneo ya makazi ya wananchi hao.




Ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami ya kilomita 1 kutoka eneo la Majengo mpaka katika daraja la Mto Amtico, wilayani Muheza mkoani Tanga, ukiendelea jana, huku barabara hiyo ikiwa imefungwa ili kuwawezesha mafundi waendelee na kazi pasipo usumbufu. **PICHA: STEVEN WILLIAM, MUHEZA**

# RC Tabora awakabidhi wazazi watoto waliopotea jijini Mbeya

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

SERIKALI mkoani Tabora imewakabidhi kwa wazazi wao watoto wawili waliokuwa wamepotea mkoani Mbeya.

Hatua hiyo inatokana na kupatikana kwa mmoja wao akiwa na mama aliyetambulika kwa jina la Hawa Ally katika Hospitali ya Wilaya ya Nzega baada ya wasamaria wema kuwa na wasiwasi na mtuhumiwa na kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi. Akikabidhi watoto hao jana, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, aliwaonya watu wote wanaohusika na vitendo vya aina hiyo, akieleza kuwa serikali itahakikisha inawachulia hatua kali za kisheria. Pia aliwataka wazazi kuwa karibu na watoto wao badala ya kuwategema wasaidizi wa kazi ndiyo watumike kuwalea muda mwingi ili kujiepusha na matatizo kama hayo.

Mwanri alilipongeza Jeshi la Polisi na wananchi kwa ushirikiano wao waliouonyesha na katika kufanikisha kupatikana kwa watoto hao wakiwa na afya njema.

Baba mzazi wa watoto hao ambaye ni mtumishi katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mashaka Juma, alisema watoto wake walipotea Desemba 28 mwaka jana. Alisema watoto wake hao wenye umri wa miaka mitano na mwaka mmoja na nusu, walipotea wakati yeye na mkewe wakiwa wamekwenda sokoni kununua mahitaji na waliporudi ndipo walipobaini hawako nyumbani kwao.

Juma alivishukuru vyombo vya habari na viongozi wa mikoa ya Mbeya na Tabora na wananchi kwa kufanikisha kupatikana kwa watoto wake, huku mama wa watoto wao, Zuhura Kaswa, akieleza namna alivyozipokea kwa mshtuko taarifa za kupatikana kwao.

Mtuhumiwa anayedaiwa kuwatorosha watoto hao mkoani Mbeya na kumtelekeza mmoja nyumbani kwa mtu eneo la Chemichemi katika Manispaa ya Tabora, Hawa Ally, anashikiliwa na Jeshi la Polisi.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Tabora, Baraka Makona, alidai mtuhumiwa huyo alimwacha mtoto mkubwa mwenye umri wa miaka mitano kwenye nyumba ya mkazi wa Chemichemi kwa madai anaenda na mdogo ili kumtafutia matibabu na kuahidi kurudi baadaye.

Alidai mtuhumiwa hakurudi siku hiyo, jambo lililomfanya mwananchi aliyetelekezewa mtoto, kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi siku iliyofuata ambayo ilikuwa ya mwaka mpya.

Baraka alidai mtuhumiwa aliendа na mdogo wake hadi Nzega na kumpeleka hospitalini kutokana na kuugua na ndipo ilipogundulika si mtoto wake na wasamaria wema kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi na mtuhumiwa kukamatwa.

Alisema baada ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kupata taarifa za kupotea kwa watoto hao, walifuatilia na kubaini mtoto mkubwa katelekezwa Manispaa ya Tabora na mdogo akipatikana Mjini Nzega.

# Kesi vigogo Acacia yapigwa kalenda

INATOKA UK. 4

Johannesburg, Afrika Kusini, Toronto (Canada) na Uingereza.

Washtakiwa Mwanyika na Lugendo pia wanadaiwa kutoa msaada katika kusimamia mkakati wa kihalifu kwa nia ya kupata faida.

Washtakiwa hao wanadaiwa kutoa tamko la uongo kwa Kamishna Generali wa TRA huko Biharamulo kwa nia ya kukwepa kulipa kodi Dola za Marekani 9,309,600 ambayo ilikuwa ni kodi iliyopaswa kulipwa kwa TRA.

Washtakiwa Mwanyika na Lugendo wanadaiwa kuwa kati ya Desemba 2009 na Desemba 31, 2018, katika maeneo tofauti ndani na nje ya Tanzania, kwa pamoja na wengine ambao hawapo mahakamani, walisaidia Mgodi wa North Mara kuhamisha Dola za Marekani 374,243,943,45, huku wakijua kuwa fedha hizo ni zao la makosa ya kughushi na kukwepa kodi.

Pia, washtakiwa hao wanadaiwa kati ya Novemba 2, 2012 na Novemba 27, 2015 huko Shinyanga, walitoa rushwa ya Sh. 718,520,001.76 kwa Hussein Kashindye, ambaye ni Mkuu wa Upelelezi Makosa ya Jinai wa Mkoa wa Shinyanga kwa lengo la kumshawishi ili aachane na uchunguzi wa makosa ya jinai yaliyokuwa yametendwa na Mgodi wa Bulyanhulu.

Katika shtaka la kughushi, washtakiwa hao wakiwa na nia ya ulaghai, wanadaiwa kughushi mkataba wa mkopo wakitaka kuonyesha kwamba Aprili 30, 2014, Kampuni ya Pangea Limited ilikubali kukopa USD 90,000,000 ikiwa na riba kutoka Benki ya Kimataifa ya Barrick huku wakijua kuwa si kweli.

Katika shtaka la kutoa nyaraka ya uongo, mshtakiwa Mwanyika anadaiwa Aprili 30, 2018 huko Benki Kuu ya Tanzania (BoT|) Ilala jijini Dar es Salaam, kwa makusudi aliwasilisha nyaraka za uongo za mkopo baina ya kampuni Mgodi wa Bulyanhulu na Barrick International Bank Corp kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa, kati ya Juni 2001 na Desemba 13, 2007, Bulyanhulu walijipatia mkopo usio na faida wa Dola za Marekani 416,100,000 kutoka Barrick.

# Waziri aagiza watumishi waongezwe kituo Nida

**Na Mwandishi Wetu,**
KIBAHA

KATIKA kwenda sambamba na siku 20 zilizoongezwa na Rais John Magufuli kusajili laini za simu kwa alama za vidole, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imetakiwa kuongeza idadi ya watumishi katika kituo cha kuchakata taarifa za waombaji nchi nzima kilichopo Kibaha mkoani Pwani.

Imeelezwa ongezeko la watumishi katika kituo hicho litasaidia kuhakikisha kila mwananchi anayekidhi vigezo kupata kitambulisho cha taifa anapatiwa kitambulisho ili kusajili laini yake ya simu.

Akizungumza baada ya kutembelea kituo hicho jana, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Dk. Anold Kihaule, kuongeza idadi ya watumishi katika kituo hicho.

Pia alimtaka kuongeza saa za kufanya kazi kutoka nane mpaka 16 kwa siku, ili kuhakikisha wananchi wanapata namba na vitambulisho baada ya nyongeza ya siku 20 ziliyotolewa na Rais Magufuli.

"Nimetembea katika vituo mbalimbali vya Nida nchi nzima, matatizo makubwa niliyoyaona ni wananchi kwenda kila siku kufuatilia kitambulisho au namba katika kituo husika, lakini wamekuwa wakipata majibu kwamba bado kipo kwenye mchakato.

"Wakati mwingine ameomba miaka mitatu iliyopita, sasa anapoteza muda na gharama kufuatilia kitambulisho, lakini nimetembelea hapa leo (jana) nimegundua uchache wa watumishi, mkurugenzi ongeza watumishi hapa.

"Naomba pia ongeza muda wa kufanya kazi, kutoka saa nane mpaka 16 kwa siku, Rais ashasema muda hautaongezwa wa usajili laini za simu, sasa wananchi wanafurika na kupata tabu vituoni huko, sisi ndiyo wawakilishi wao, lazima tuwasemee na mkuu wa nchi ashatoa maelekezo, sasa ni utekelezaji tu," aliagiza.

Akizungumza katika ziara hiyo ya Masauni, Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Dk. Kihaule, alisema watayatekeleza maagizo hayo ya serikali, huku akiwataka wananchi ambao tayari wana namba za utambulisho waende kusajili laini zao ili kwenda sambamba na muda ulioongezwa na Rais Magufuli.

"Jumla ya watu milioni 7.6 tayari wana namba za utambulisho nchi nzima na kila siku tunaendelea kutoa namba hizo sehemu mbalimbali nchini na mnaweza kuona kwa Dar es Salaam katika Viwanja vya Mnazi Mmoja tunatoa namba pale na ni zoezi la siku zote za wiki, hatuna sikukuu wala siku za mwisho za wiki," alisema.



Mwendesha bodaboda jana, akifunga bomba la maji lililokuwa limekatika na kumwaga maji mengi katika Mtaa wa Nyahanga Sokoni, Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga. **PICHA NA SHABAN NJIA**

# Raia Uingereza akiri uhujumu, ahukumiwa

INATOKA UK. 3

Jabir, alidai mteja wake ni mkosaji wa kwanza, hajaisumbua mahakama kwa kukiri makosa yake mwenyewe na kwamba anategemewa na familia yake.

Wakili huyo pia alidai mshtakiwa huyo ana tatizo la uti wa mgongo na mfumo wa upumuaji, hivyo aliomba mahakama impe adhabu ndogo ya faini.

Awali, akisoma maelezo ya awali, Wakili wa Serikali, Sylvia Mitanto, alidai Banton ni mfanyabiashara na makazi yake ni London, Uingereza na kwamba alisafiri kuja nchini kwa ndege ya Emirates kupitia Dubai.

Alidai Desemba 4, 2019, alitoka Rwanda kuja nchini kufanya utalii na kusalimia rafiki zake na kwamba Desemba 6, 2019, akiwa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, alikutwa akisafirisha madini ya dhahabu bila kibali.

Alidai Tume ya Madini iliyafanyia tathmini na kubaini madini hayo yana uzito wa gramu 300.7 yakiwa na thamani ya Sh. 29,067,318.

Banton alifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza Desemba 20, mwaka jana, akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 136/2019.

Katika mashtaka hayo, ilidaiwa Banton alisafirisha madini ya dhahabu yenye uzito wa gramu 300.7 yakiwa na thamani ya Sh. 29,067,318 bila kuwa na leseni kutoka mamlaka husika.

Pia, ilidaiwa kuwa siku na eneo hilo, mshtakiwa alikutwa akimiliki madini hayo, ambayo ni mali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bila kuwa na kibali kutoka mamlaka husika.




Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Victoria, Ezekeiah Wenje, akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi ya kanda jijini Mwanza, kulia ni Katibu wa chama hicho, Rehema Mkoha. **PICHA NA ELIZABETH FAUSTINE**

# Sekta ya afya yapewa mbinu kukabili kimeta

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAFANYAKAZI wa Sekta ya Afya wilayani Monduli wapatao 200, wamepatiwa mafunzo ya kukabiliana na magojwa ya mlipuko kama vile kimeta na kipindupindu, yanayoiandama wilaya hiyo kutokana na mvua ya mafuriko.

Mafunzo hayo yameendeshwa kwa siku tisa katika Mji wa Mto wa Mbu wilayani humo na wadau wa afya kutoka Taasisi ya Tandia ya Ujerumani.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi wakati akifunga mafunzo hayo, mratibu wa dharura na magonjwa ya mlipuko wilayani humo, Dk. Joel Nkika alisema semina hiyo ililenga utayari kwa wauguzi na madaktari katika kupambana na magonjwa ya dharura na milipuko.

"Magonjwa ya milipuko kama kimeta na kipindupindu yamekuwa yakijitokeza sana wilayani kwetu na kusababisha vifo kwa wanyama na binadamu. Hivyo, mafunzo haya ya kujiweka utayari, yatatusaidia sana kupata elimu ya kukabiliana na magonjwa haya," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Tandia, Regina Meissner, alisema taasisi yake imekuwa ikisaidia sekta za afya na elimu wilayani humo tangu mwaka 2015 na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza vikwazo vya afya kwa wakazi wa wilaya hiyo.

Alisema pamoja na kufadhili mafunzo hayo, taasisi yake pia imesaidia ujenzi wa zahanati kwa kujenga vyumba vya kujifungulia na matangi ya maji katika zahanati mbalimbali zilizoko Mbuyuni wilayani humo.

"Tumejikita zaidi katika Wilaya ya Monduli baada ya kubaini kuwa familia nyingi za kifugaji zina matatizo makubwa ya kukumbwa na magonjwa ya milipuko na uhaba wa vyumba vya kujifungulia katika zahanati. Tuna mpango wa kwenda katika wilaya zingine kusaidia sekta ya afya," alisema.

Dk. Emmanuel Msofe, aliyepata mafunzo hayo alisema: "Kwa kweli, kabla ya mafunzo haya, uelewa wangu ulikuwa mdogo, ila kwa sasa nimepata uelewa zaidi juu ya matumizi ya dawa na vifaa na namna ya kujikinga wakati nikihudumia mgonjwa."

Mratibu wa mafunzo hayo, Joyce Shanghai, alisema tangu Taasisi ya Tandia iingie wilayani Monduli mwaka 2015, imeendesha mafunzo kwa idara mbalimbali za afya wakiwamo wahudumu wa vyumba vya kuhifadhi maiti, wauguzi, maofisa afya, idara ya maabara na madaktari na kupunguza maambukizo ya

# Mabadiliko tabianchi yazidi kuumiza vichwa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WADAU wa kilimo na wakulima wa zao la maharage, wametakiwa kushirikiana na serikali kupambana na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa, ili wazalishe mazao yenye tija.

Akizungumza jijini Arusha juzi wakati akifungua warsha ya siku mbili ya wadau wa kilimo iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) kupitia mradi wa Afrika Mashariki wa Kilimo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega, aliwahimiza washiriki hao, kushirikiana na serikali zao ili kukabiliana na matatizo yaliyopo.

Alisema mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa ni kikwazo kwa nchi zote duniani, na yamesababisha madhara makubwa katika shughuli za kiuchumi.

Kwitega alisema kupitia mradi huo wa SNV, ni vema wakulima na wadau wengine wa kilimo kuweka mikakati kabambe, ili wakulima na wadau wa zao hilo, wakabiliane na athari zinazojitokeza pindi mvua inapokosekana au kupungua.

Alisema zao la maharage ni muhimu kwa chakula na biashara, hivyo ni lazima kuweka mikakati ya kuongeza uzalishaji wake hasa wakati huu wa mabadiliko ya tabianchi, yanayosababisha ukosefu wa mvua za uhakika na kujitokeza kwa joto kali.

Msimamizi wa mradi huo, Godfrey Kabuka, alisema uko katika nchi zaidi ya 15 za Afrika na pia uko kwenye nchi zaidi ya 30 duniani, ukilenga kusaidia wakulima wadogo ili wajikwamue kimaisha kwa kuwapatia mbinu za kukabiliana na mabadiliko yanayojitokeza.

"Hapa tunawahimiza sana matumizi ya mbegu zilizo sahihi zinazotolewa na wataalamu wetu na kuepuka kutumia mbegu zilizotumika miaka ya nyuma au za kienyeji," alisema.

Alisema mradi huo unatekelezwa kwa miaka mitano kwa gharama ya Euro milioni 39 zilizotolewa na Shirika la Maendeleo la Uholanzi.

Alisema warsha hiyo imekutanisha wakulima wadogo wa zao la maharage, wasambazaji wa pembejeo, watafiti wa kilimo, taasisi za fedha na wadau wengine wa kilimo kutoka nchi tatu za Afrika Mashariki unakotekelezwa mradi huo.

Mwakilishi kutoka Chuo Kikuu cha Uholanzi, Annamarie Groot, alisema mabadiliko ya tabianchi yanahitaji nguvu ya pamoja kuyashughulikia na siyo mmoja mmoja au nchi moja kwa faida ya kizazi kijacho.

# Wanufaika mamilioni mikopo halmashauri

**Na Mwandishi Wetu,**
SIMANJIRO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara imevipatia vikundi 71 vya wanawake, vijana na walemavu Sh. milioni 230.8 za mikopo kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ili kuvinyanyua kiuchumi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Asia Ngalisoni, akizungumza jana kuhusu mikopo hiyo iliyotolewa mwaka jana, alisema kati ya vikundi hivyo, vya kata ni 14 vilivyonufaika na mkopo huo.

Ngalisoni alisema mkopo huo ulitolewa kwa vikundi 59 vya wanawake 1,531, vikundi tisa vya vijana 238 na vikundi vitatu vya walemavu 57.

Alisema hadi Mei mwaka jana, halmashauri ilikuwa imekusanya Sh. bilioni 1.7 ikiwamo mapato ya ndani na marejesho ya fedha za vikundi vilivyokopeshwa awali.

"Mfuko huu unawanufaisha wananchi waliojiunga katika vikundi vyenye shughuli za ujasiriamali au vinavyokusudia kuanzisha shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, alisema mkopo unaotolewa hauna riba, hivyo vikundi hivyo vinapaswa kuchukua mikopo hiyo na kurejesha kiasi kile kile walichokopa.

"Nitoe wito kwa vikundi vyote vilivyokopeshwa na halmashauri, virejeshe fedha hizo kwa wakati, ili wengine nao wakope na kujikwamua kiuchumi," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Jackson Sipitieck, alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Yefred Myenzi, kwa kusimamia ipasavyo na kufanikisha utolewaji wa mikopo hiyo.

"Wakati halmashauri zingine zikisuasua kufanikisha mikopo, sisi Simanjiro tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwani tunatoa mikopo hadi fedha nyingine zimebaki," alitamba.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Myenzi, alitoa wito kwa vijana wa eneo hilo kuchangamkia fursa hiyo, akibainisha kuwa mwitikio wa kundi hilo bado ni mdogo.

"Zile fedha zenu vijana za asilimia nne mnazopaswa kupewa hamjazichukua, hivyo vijana wa Simanjiro mnapaswa kubadilika ili mnufaike kupitia mikopo hii tunayoitoa," alisema.





Msukuma mkokoteni akiwa amelala uzingizi baada ya kukosa mizingo ya kubeba toka kwa wateja kama alivyokutwa katika Mtaa wa Uhindini jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Vijana wapewa mchongo wa kuinuka kiuchumi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIJANA wametakiwa kutoogopa kujiunga kwenye vikundi vya uzalishaji mali kwa kutumia fursa za mikopo inayotolewa na halmashauri ili kujikwamua kiuchumi.

Hayo yalibainishwa jana na Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Dodoma, Sharifa Nabalaganya, wakati akifungua mkutano wa kuunda mtandao wa vikundi vya vijana.

Alisema vijana hawatakiwi kuogopa kujiunga kwenye vikundi bali wavikimbilie na kuvifanya mkombozi wao kiuchumi.

Pia alisema ni vyema kama wataungana na kupaza sauti zao ikiwa ni pamoja na kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za maendeleo kama vile uzalishaji mali.

"Serikali iko Dodoma na Rais John Magufuli tayari amehamia Dodoma. Lazima tujitume kuonyesha vijana tunaweza kulitumikia taifa kwenye shughuli mbalimbali kama vile kilimo, ufugaji na ujasiriamali," alisema.

Nabalaganya alisema kumekuwa na changamoto kubwa za ushiriki wa vijana kwenye masuala mbalimbali kutokana na kutokuwa na mtandao unaowaunganisha tofauti na ilivyo kwa wanawake na watu wenye ulemavu.

Pia alisema serikali ilishatoa agizo la kila halmashauri kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu lakini changamoto kubwa kwa vijana ni miradi mingi iliyopo si halisi.

"Kuna changamoto nyingine kubwa kwa vijana kutorudisha fedha za mikopo kwa wakati. Fedha zinazotolewa kwa ajili ya mikopo zinatakiwa zirudishwe kwa wakati ili watu wengine wakope," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2015/16 kuna miradi mingi ya vijana bado inadaiwa kwa kuwa imeshindwa kurejeshwa kwa wakati tofauti na urejeshaji mwingine unaofanywa na vikundi vya wanawake na wenye ulemavu.

"Miradi mingi ya vijana si halisi. Tunataka kuona mnakuwa na miradi ya mfano ili watu wengine wajifunze kutoka kwenu. Mnatakiwa kuchangamkia sekta ya kilimo ambayo inaleta tija kubwa sana kwenye miradi mingi kikiwamo kilimo cha mboga, matunda, nyanya na mazao mengine," alisema.

Ofisa huyo alisema kuna fursa nyingi ambazo vijana hawazichangamkii hasa kipindi hiki ambacho Dodoma imekuwa makao makuu ya nchi kwa kuwa kuna mwingiliano mkubwa wa watu na biashara nyingi zinafanyika.

"Dodoma ina mapato mengi ya ndani kuliko maeneo mengine, hivyo ni vizuri mikopo kwa vijana wazalishaji mali ikachangamkiwa," alisema.

Pia aliwataka kutoishia kwenye uzalishaji tu bali kuzalisha bidhaa zinazokidhi viwango na zenye ubora unaotakiwa kwenye sok

# Takukuru yaokoa mamilioni kupigwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Dodoma imeokoa Sh. milioni 919.846 za miradi 103 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. bilioni 134 inayotekelezwa jijini Dodoma.

Miradi hiyo inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali mkoani hapa ni ile ya elimu, ujenzi wa miundombinu, afya na maji.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema wameokoa fedha hizo katika miradi hiyo kwa kipindi cha mwaka jana zilizodhibitiwa katika urekebishwaji wa mifumo ya utekelezaji wa miradi hiyo iliofanyiwa udanganyifu. Alisema fedha hizo zimerejeshwa katika halmashauri mbalimbali kwa ajili ya kuendelea na shughuli nyingine za maendeleo. "Tumefanikiwa kuokoa kiasi hiko cha fedha kutokana na ufuatiliaji wa miradi ikiwamo urekebishaji wa mifumo iliyotumika na kusababisha kufanya udanganyifu," alisema Kibwengo.

Alifafanua kuwa mwaka huu wanaendelea kujipanga katika ufuatiliaji na uchambuaji wa miradi mbalimbali ambayo itaendelea kutekelezwa mkoani hapa.

Alisema lengo lao ni kuona miradi ya wananchi inatekelezwa vizuri ili maendeleo yaonekane kupitia miradi hiyo ambayo inaendelea kutekelezwa. Kibwengo pia alisema kwa upande wa kesi ambazo zimewafikia mezani ni 26 lakini kati ya hizo tisa wameshinda, mbili wamepoteza na moja wameikatia rufani.

Kuhusu mafanikio, mbali alisema wamefungua klabu za wapinga rushwa 203 ambazo zote zinatoa elimu katika shule za msingi, sekondari na vyuoni jinsi ya kuepuka kutoa au kupokea rushwa.

Alisema klabu hizo zimekuwa msaada mkubwa hususani kuwaelimisha wanafunzi ambao hawajui nini maana ya rushwa.

"Tumejipanga kuhakikisha kila wilaya mkoani hapa shule zinakuwa na klabu za wapingwa rushwa. Lengo ni kuona kila mmoja anakuwa na elimu kuhusu rushwa," alisema Kibwengo.

# Polisi yapewa muda kukamilisha ujenzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi limetakiwa hadi kufikia Januari 31, mwaka huu, liwe limekabidhi mradi wa ujenzi wa jengo la makao makuu ya Jeshi la Zimamoto na Ukoaji lenye thamani ya Sh. bilioni 2.65 ambalo liko hatua za mwisho kukamilika.

Jeshi hilo linatakiwa kuanza kutumia jengo hilo la makao makuu kuanzia Februari 10, mwaka huu. Jengo hilo hadi sasa ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 90.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa wakati wa ziara ya kutembelea jengo hilo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ramadhan Kailima, aliagiza jengo hilo hadi Januari 31, liwe linekamilika ili jeshi hilo lianze kulitumia.

Kailima alisema Februari 10, mwaka huu, wanapaswa kuwa wamehamia kwa ajili ya kuanza rasmi shughuli za utendaji za kila siku.

"Jengo hili limejengwa kwa kutumia 'force account' na hii imesaidia kupunguza gharama za ujenzi wa kawaida," alisema Kailima.

Alisema wanamshukuru Rais John Magufuli kwa kulijali Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutokana na kuwasaidia fedha hizo ambazo zimechangia kwa kiasi kikubwa kukamilika kwa jengo hilo lenye ghorofa nne.

Kwa mujibu wa Kailima, wana kila sababu ya kujivunia serikali kwa sababu inalipa kipaumbele jeshi hilo kwa kulijengea ofisi kama moja ya motisha ya ufanyaji kazi.

Naye Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, (SSP) Constantine Kiwone, ambaye ndiye msimamizi wa ujenzi huo, alisema ujenzi huo utakuwa umekamilika kama ilivyoagizwa.

# Mhadhiri ashangaa vijana kuombaomba

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MHADHIRI Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Nelson Mandela cha jijini Arusha, Dk. Eliamani Laltaika, ameeleza kushangazwa kwake na idadi kubwa ya vijana kugeuka ombaomba, wakati ziko fursa nyingi za kujipatia kipato halali.

Badala yake, amewataka kuacha tabia hiyo, kujifunza kwa vitendo na kuondoa uoga wa kuanzisha biashara au kubuni kazi ambazo zitawasaidia kujipatia kipato ambacho kitawawezesha kuendesha familia zao bila kuwa tegemezi.

Dk. Laltaika ambaye ni Mkufunzi wa Ubunifu kwa Vijana, alikuwa akizungumza jana wakati wa kufunga Kongamano la Fursa kwa Wasanii Wilaya ya Siha ambalo liliandaliwa na Mtandao wa Wasanii wa Injili Tanzania (Tagoane).

"Mnao uwezo wa kujiunga na kuomba kupatiwa mafunzo ya kuwaongezea uwezo wa kuthubutu katika masuala ya muziki na ujasiriamali. Mkijengewa uwezo na mkaingia katika biashara, mtaongeza ushindani na nchi nyingine duniani zilizoendelea kiuchumi.

"Shida yetu kubwa ni kwamba bado wengi wetu, hatuna ujasiri wa kujitegemea wenyewe na tuna imani potofu za kushindwa kumiliki biashara au kampuni zetu za muziki na badala yake tunasubiri kila kitu serikali ifanye, haiwezekani," alisema.

Dk. Laltaika alitumia fursa hiyo kuwataka wasanii kuwa na ubunifu katika kazi zao ambazo wanazifanya.

"Msanii yeyote ambaye anakuwa na kipaji halafu si mbunifu ni sawa na kuwa mlinzi wa shamba la bibi. Unawalimia watu halafu watu wengine wanakuja wanachukua akili yako na kwenda kuitanyia kazi huku wewe ukiendelea kutaabika," alisema.

Pia alisema kuna aina mbalimbali za ubunifu, kuna ubunifu wa kibiashara, ubunifu wa kijamii, ubunifu wa kutunga nyimbo, kuandika vitabu, uchoraji na ubunifu wa kisanii, hivyo wasanii ni lazima wazingatie hizo kanuni kwani bila kufanya hivyo wasitarajia kama wanaweza kufanikiwa.

Kwa upande wake, Rais wa Tagoane, Dk. Godwin Maimu, aliwahimiza wasanii kufanya kazi kwa nidhamu na kwamba hata hao wasanii ambao walisha tangulia mbele za haki, huku nyimbo zao zikiendelea kupigwa kila kona walifanya kazi nzuri ndio maana wanaendelea kukumbukwa ni kwa sababu walifanya kazi nzuri.

Awali, Ofisa Utamaduni Mkoa wa Arusha, Benson Maneno, akizungumza kwa niaba ya Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa la Taifa (Basata), Godfrey Mngereza, alisema serikali iko mbioni kubadilisha sheria iliyounda Chama cha Hakimiliki Tanzania (Cosota) ili kumnufaisha kila msanii hata kama atakuwa ametangulia mbele za haki.

# Kikongwe kortini tuhuma ubakaji

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

KIKONGWE mwenye umri wa miaka 80, Obed Ndosi, maarufu kama Ulong'a, mkazi wa Kijiji cha Masama Mbweera, amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, akikabiliwa na shtaka la kumbaka mwanafunzi wa darasa la sita.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, Ulong'a anadaiwa kutenda kosa hilo kinyume cha kifungu 130 (1), (2), (e) na 131 (1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 cha Sheria iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2002.

Katika hati ya mashtaka iliyosomwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Lobulu Mbise, inadaiwa kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo katika Kijiji cha Masama Mbweera Desemba 8, mwaka jana kwa nyakati tofauti. Mwanafunzi huyo wa darasa la sita (jina linahifadhiwa) anayedaiwa kubakwa kwa nyakati tofauti na Ulong'a ana umri wa miaka 13.

Kesi hiyo namba 333 ya mwaka 2019, inasikilizwa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Devotha Msofe.

Baada ya mshtakiwa kusomewa mashtaka hayo, alikana kutenda kosa hilo na hakimu aliahirisha shauri hilo hadi Januari 29, mwaka huu, kesi hiyo itakapotajwa tena.

Upelelezi wa shauri hilo kwa mujibu wa mwendesha mashtaka wa serikali, bado haujakamilika.

Hakimu huyo alisema dhamana ya mshtakiwa huyo iko wazi na kwamba alipaswa kuweka bondi ya Sh. milioni tano. Baada ya maelezo hayo ya Hakimu Mkazi, mshtakiwa huyo alitimiza matakwa ya dhamana.



Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa (kulia), wakibadilishana mawazo na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kilolo, Kilian Myenzi, kabla ya mbunge huyo kufanya mkutano na waandishi wa habari katika Mtaa wa Uhindini Manispaa ya Iringa jana. Mbunge atafanya mkutano wa hadhara Jumapili Januari 5, katika Viwanja vya Mlandege Mjini Iringa. **PICHA NA FRIDAY SIMBAYA**

# Wafanya utafiti uzalishaji mpunga

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

JOPO la wataalamu wa kilimo kutoka Chuo cha Mafunzo ya Kilimo na Utafiti wa Mpunga Kilimanjaro (KATC) na Kituo cha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari) cha Ifakara mkoani Morogoro, wameanza utafiti wa matumizi bora ya pembejeo na mbegu bora katika skimu ya umwagiliaji wa mpunga ya Kivulini iliyoko wilayani Mwanga.

Wataalamu hao, pamoja na mambo mengine, wanataka kupunguza hasara wanayopata wakulima katika kilimo cha mpunga.

Jana, Ofisa Kilimo anayesimamia skimu hiyo, Michael Kimaro, alisema kwa sasa wameanza utafiti huo ili kuwasaidia wakulima kutumia pembejeo chache kuzalisha mazao yenye tija kwa kutumia mbegu bora na matumizi sahihi ya mbolea.

"Zaidi ya wakulima 1,800 wa skimu ya umwagiliaji wa kilimo cha mpunga Kivulini, wanakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya umwagiliaji na miundombinu ya barabara. Kimsingi hali hiyo imekuwa ikichangia wakulima wengi kushindwa kulima kilimo cha kisasa na chenye tija kutokana na gharama kubwa za uzalishaji wa mpunga," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo, wataalamu wa kilimo kutoka KATC na Tari Ifakara, wanafanya tafiti za matumizi bora ya pembejeo na mbegu bora katika skimu hiyo.

Kwa mujibu wa Kimaro, changamoto kubwa iliyopo kwa sasa ni ya wakulima kushindwa kutumia mbinu bora za kilimo na miundombinu ya umwagiliaji, ambayo imekuwa ikipoteza maji mengi kipindi cha umwagiliaji.

Aidha, alisema skimu hiyo yenye ukubwa wa hekta 920, kati yake hekta 410 pekee ndiyo zilizojengewa mifereji.


Hata hivyo, baadhi ya miundombinu hiyo tayari imeanza kuharibika na kwamba hekta 510 ndizo zinazotumia mifereji ya asili kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na wakulima wamekuwa wakipata shida ya kufanyia usafi mifereji hiyo mara kwa mara.

Naye Mtafiti wa Kilimo kutoka Tari Ifakara, Dk. Jerome Mgase, alisema kwa sasa wameanza jitihada za kuhakikisha wakulima wanatumia pembejeo chache kuzalisha mazao yenye tija kwa kutumia mbegu bora na matumizi sahihi ya mbolea.

Alisema kwa sasa mafanikio yameanza kuonekana kwa baadhi ya maeneo ambayo tafiti hizo zimeshafanyika ili kuongeza kipato na chakula kwa wakulima kufikia ubora wa kitaifa na kimataifa.

Baadhi ya wakulima, waliozungumza na Nipashe katika skimu hiyo, walisema wamekuwa wakitumia gharama kubwa katika kilimo cha mpunga kutokana na kutumia matumizi ya pembejeo nyingi kwenye zao hilo.

Mmoja wa wakulima hao, Mwanganga Kipande, alisema matumizi hayo makubwa ya pembejeo na mbolea yamekuwa yakiwasababishia hasara kubwa baada ya mavuno, hivyo wanaiomba serikali kutoa ruzuku za pembejeo, ujenzi na ukarabati ya miundombinu ya umwagiliaji na barabara.





Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, akimkabidhi tiketi ya safari mwanafunzi, Abdul Wahid anayetarajiwa kwenda nchini Algeria kesho, kwa ajili ya masomo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR**

# Shein asisitiza ardhi kwa kilimo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema ardhi iliyotengwa kwa ajili ya kilimo Zanzibar ni vyema ikatumika kwa ajili ya shughuli hiyo na si vinginevyo.

Dk. Shein aliyasema hayo jana wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji huko Kinyasini Kisongoni, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema kilimo ni ardhi, hivyo endapo ardhi haitokuwapo kilimo hakitafanyika na hata historia ya Zanzibar inaonyesha wafanyakazi na wakulima walishindwa kulima kabla ya Mapinduzi kutokana na kunyang'anywa ardhi yao.

Alisema Zanzibar hivi sasa ardhi imekuwa ndogo kutokana na matumizi mabaya ya rasilimali hiyo yanayofanywa na baadhi ya wananchi.

Kuhusu historia ya ardhi, Dk. Shein alisema miaka mingi kabla ya Mapinduzi matukufu ya Januari 12, 1964 Wazanzibari waliteseka katika kutafuta ardhi na pale walipotaka kulima iliwalazimu wakapige magoti kwa wakoloni.

Dk. Shein alisema mashamba 745 yalihodhiwa na watu wachache kabla ya Mapinduzi, huku mmoja akiwa na mashamba 300 pekee yake na mtu wa chini alikuwa na mashamba matatu na waliuziana kwa matabaka na hakukuwa na Mwafrika aliyekuwa na shamba.

"Wananchi wa Zanzibar hawakuwa na shamba la kulima na badala yake aliyekuwa akitaka kulima alitakiwa kujiunga na Chama cha Hizbu hali ambayo Chama cha Afro Shiraz (ASP) kilinunua shamba la Kilombero ambalo lilinunuliwa chini ya uongozi wa marehemu mzee (Abeid Amaan Karume)," alisema.

Alisema Novemba 11, 1964 Mzee Karume aligawa eka tatu tatu kwa wananchi ambazo walitakiwa walime katika maisha yao yote na si wajenge au wakate viwanja. Dk. Shein alisema azma ya Serikali ya Awamu ya Saba ni kuongeza idadi ya matrekta ili wananchi walima kwa ufanisi zaidi na kuwasaidia wakulima wa mpunga hasa kinamama ambao wamekuwa wakifanya kazi kubwa katika kilimo hicho.

Alisema serikali imekuwa ikiongeza mazingira mazuri zaidi hasa katika kilimo cha mpunga ili kulima kwa faida. Pia alisema juhudi zimechukuliwa katika kuhakikisha kiwanda cha matreka kinafufuliwa.

Rais Dk. Shein aliitaka Wizara ya Kilimo kuongeza kasi kwenye kazi zao na kuondoa mivutano miongoni mwao na wawe wamoja na pale wanapopewa maelekezo na serikali wayafanyie kazi na wasishindane kwa kuwa ushindani hauna tija.

Naye Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, alisema kuwa azma ya wizara hiyo ni kuhakikisha kilimo kinakuwa na tija kubwa, huku akieleza agizo la serikali katika sekta ya kilimo.

Alisema kuwa wizara hiyo itaendelea kuwatumia wataalamu hao katika sekta ya kilimo hasa katika kilimo cha mpunga, huku akisisitiza hatua zitakazochukuliwa ili wakulima walime kwa faida na thamani.

# Kituo cha utalii kuongeza ajira

**Na Rahma Suleimam,**
ZANZIBAR

KITUO cha Utalii kinachojengwa Bungi, Wilaya ya Kati, kinatarajiwa kuupa taswira mpya Mkoa wa Kusini Unguja ili kuvutia watalii wengi na kutoa fursa za ajira kwa wakazi wa mkoa huo.

Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, alisema jana kuwa hatua hiyo ni muhimu kwa ukuaji wa utalii nchini ambao kwa sasa ndio tegemeo kubwa la kuingiza fedha za kigeni na kuinua uchumi. Akizungumza na wananchi baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo hicho sambamba na kulizindua kasri la Bi. Khole lililojengwa upya, Spika Zuberi alisema dhamira ya serikali ni kutanua wigo wa ushiriki wa wananchi katika harakati za ukuzaji wa utalii. Hafla hiyo ni sehemu ya shamra shamra za maadhimisho ya Miaka 56 ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964 yaliyowakomboa wananchi wa Zanzibar kutoka katika utawala wa wakoloni.

Zuberi alisema ili kuwawezesha wananchi kutekeleza dhana ya utalii kwa wote, serikali imeamua kuyafufua maeneo na majengo yote ya kihistoria kwa lengo la kuitangaza Zanzibar kimataifa.

Alisema ni vyema Wazanzibari waijue historia ya nchi yao, hivyo kujengwa kwa maeneo hayo ni fursa kwao ya kuyatembelea na kujua nchi ilikotoka na mnasaba wake na watawala wa kale.

Hata hivyo, aliwasisitiza wananchi wa Mkoa wa Kusini Unguja na wengine, kuhakikisha wanayalinda vyema maeneo hayo na kutoyaharibu ili yaweze kudumu na kubaki katika haiba yake kwa miaka mingi ijayo na kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.

"Serikali inatumia gharama kubwa kuyatengeneza maeneo na majengo ya kale kwa ajili ya ustawi wa wananchi, hivyo ni jukumu letu sote kuyalinda na kuyatunza kwani faida yake itawafaa watoto na wajukuu zetu hapo baadaye," alisema. Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Khadija Bakari Juma, alisema ujenzi wa kituo cha utalii Bungi utakapokamilika, utaongeza maeneo ya burudani kwa

wananchi na wageni ikizingatiwa idadi ya watu inaongezeka hivyo kuna mahitaji makubwa ya maeneo mapya ya mapumziko.

Alisema kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia 2017, Serikali ya Mapinduzi

Zanzibar imetenga fedha maalum kwa ajili ya mradi wa kuimarisha maeneo ya kihistoria Unguja na Pemba. Alisema katika mwaka wa fedha 2017/18 serikali imetoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuimarisha maeneo ya kihistoria kwa Bi. Khole Bungi na Mwinyi Mkuu, Dunga.

Aidha, alisema katika mwaka 2018/19 Sh. milioni 850 zilitolewa ili kuyaimarisha maeneo ya kihistoria ya Fukuchani, Unguja na Mkama Ndume, Pemba, huku mwaka 2019/20 serikali ikitoa Sh. bilioni 2.4 kwa kazi kama hiyo kwa maeneo ya Mvuleni, Unguja, Mwinyi Mkuu na Mkama Ndume awamu ya pili.

# Wanaokwenda kusoma Algeria wapewa neno

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma,amewataka wanafunzi wanaokwenda kusoma nchini Ageria kuitumia vyema fursa walioipata na kuwa na bidii katika masomo yao ili kufikia malengo yao waliyokusudia.

Akizungumza jana katika hafla ya kuwakabidhi tiketi na kuwaaga wanafunzi hao, alisema wanafunzi hao wemepata fursa za masomo nje ya nchi ikiwa ni sehemu ya matunda ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

Waziri huyo alisema wanafunzi hao wanapaswa kuendelea kutunza mila, silka na utamaduni wa nchi yao na kutokubali kuwa wadhaifu katika suala lolote lililo kinyume cha walililoliendea.

Aidha, aliwapongeza kwa kupata nafasi hiyo ya masomo na kuwataka kuwa wazalendo kwa kurejea nchini watakapomaliza masomo yao ili kulitumikia taifa.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Elimu ya Juu, Aida Maoulid Juma, alisema serikali ya Algeria imegharamia kila kitu na Serikali ya Mapinduzi

Zanzibar ikaamua kuwagharamia nauli ya mkopo usiokuwa na riba ili kuhakikisha wanafunzi hao wanaipata fursa hiyo.

Kwa upande wao, wanafunzi hao wanaokwenda nchini Algeria, walimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, kwa kuendelea kuinua sekta ya elimu pamoja na kupigania upatikanaji wa fursa za kimasomo nje ya nchi.

Wanafunzi tisa wamekabidhiwa tiketi na wanatarajiwa kundoka nchini kesho kwenda Algeria kuanza masomo ya elimu ya juu.



**DJ CUPPY AANZA MWAKA AKIWA SINGO** Soma UK.20

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT
JUMAMOSI JANUARI 4, 2020



WAREMBO ZAIDI AFRIKA

# Jokate, Jacqueline Mengi waongoza

BASI SAWA

## Ommy Dimpoz amsifu Nandy picha za utata

MWANAMUZIKI Ommy Dimpoz, ameamua kutoa ufafanuzi kuhusu picha zilizosambaa zikimwonesha akiwa na msanii mwenzake Nandy katika mapozi ya kimahaba.

Dimpoz ameongea na Millardayo kwamba picha hizo zilichukuliwa wakati wakiandaa video ya ngoma mpya ambayo wasanii hao wamefanya kazi pamoja.

"Ukweli ni kwamba picha hizo zinatoka kwenye vipande vya goma yangu mpya niliyomshirikisha Nandy ambayo itadondoshwa siku yoyote wiki hii," amesema Dimpoz.



## Nana aamua kufichua siri

WALE waliodai kwamba Rayvanny amekolea kwa penzi la mnogeshaji wa video za muziki, Nana, watakuwa wamkosea.

Hivi karibuni mrembo huyo aliyefanya vyema katika kibao cha Rayvanny 'I Love You' ametupia picha ikimwonesha mume wake wa ndoa.

Inaelezwa Nana na mume wake anayejulikana kwa jina la Lee, walifunga ndoa mwaka jana.





HAWASHIKIKI

## Harmonize, Nandy ni sauti nyingine

JUKWAA linaloaminika kwa huduma ya kupakua muziki barani Afrika, Boomplay, imewataja wanamuziki Diamond Platnumz, Harmonize na Nandy, kuwa nyimbo zao zinaongoza kusikilizwa Tanzania.


Taarifa hiyo iliyowekwa kwenye ripoti maalumu kuhusu muziki mwaka 2019, imeegemea zaidi katika takwimu kutokana na jukwaa hilo kuwa na wafuasi zaidi ya milioni 60.

Boomplay inahifadhi aina tofauti za nyimbo, idadi yake ni zaidi ya milioni 20, ambazo zinapatikana kwenye mtandao.

Katika orodha hiyo, Diamond anashika nafasi ya kwanza, namba mbili imenyakuliwa na mwanadada Nandy na ya tatu imekwenda kwa Harmonize.

Wasanii wengine waliofuatia ni Rayvanny, kundi la Yamoto, Aslay Mbosso, Jux na Lava.

Boomplay pia imetoa taarifa za mwenendo na tabia za namna muziki unavyosikilizwa Tanzania. Katika taarifa hiyo maalumu, Nyimbo za injili (Gospel) zimeonekana kusikilizwa zaidi na kufuatiwa na miondoko ya Bongo Fleva, kisha Afrobeats inashika namba tatu, huku ya nne na tano zikishikwa na Hip Hop & Rap pamoja na Reggae.




Ir
W
vy

MBU...
Irad...
2020...
Ira...
naks...
(bai...
tham...
Ar...
wak...
nje y...
wa r...
mko...
Ka...
wa k...
ya k...
Shop...
Aver...
Mwa...

INSTA-TWITTER






**Ndugu** zangu embu kila mmoja ajipige kifua huku akisema "Mimi tangu nizaliwe sijawahi kuchepuka" Mi leo sitaweza kifua kinaniuma-**Idriss Sultan.**



**Siku** zote nime... kuwa nikiamin... kwamba mimi... ni mwanamke mwenye nguvu. Mpaka ha... nilipofikia, nimepitia ... sana. muda mwingine ... kata tamaa kabisa. Na... shukuru Mungu kwa k... jambo, nanyi pia mas... wangu. Mwaka huu 20... naamini nitafanya kit... ajiri yenu-**Ebitoke.**



## ada aomba Watanzania kupenda ya nyumbani

UNIFU wa mavazi, Irada Mtonga, anayemiliki lebo ya a Style, amewataka Watanzania kuufanya mwaka 0 kuwa wa bidhaa za nyumbani.

ada ambaye amejikita zaidi katika kuyaongezea hi mavazi ya staha yanayovaliwa na wanawake bui), amesema kununua bidhaa za nyumbani kutaipa nani kubwa nchi kwa kuongeza mapato.

nesema kwa muda mrefu Watanzania wamekuwa ipenda kuvalia nguo zilizobuniwa au kutengenezwa ya nchi, lakini uwepo wa idadi kubwa ya wabunifu ndani ni muda sasa wa Watanzania kuwaunga no.

tika kuhakikisha Watanzania wanapata wasaha kununua mavazi hayo, ameandaa siku maalumu uuza na kuonyesha mavazi yake ijulikanayo kama N' Dine itakayofanyika katika bustani ya Garden nue, katika ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa wa alimu Nyerere.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

UNASEMAAA...

### UMESHACHELEWA

# Uwoya awauliza kama mtoto sasa itakuwaje?

NI bumbuwazi! Baadhi ya wanamitandao wamejikuta wameduwaa, baada ya mwigizaji wa Bongo Muvi, kuzungumza maneno yanayoashiria tayari ametoka kimapenzi na mwanamuziki Rayvanny.

Mshangao huo umetokana na maneno ya Uwoya katika ukurasa wake wa Instagram, akimwambia shabiki wake kwamba amechelewa kumwonya asitembee na mwanamuziki huyo.

Uwoya alitupia picha ikiwaonyesha akiwa yeye na Rayvanny, ndipo shabiki mmoja alipotoa angalizo kwamba asije akatembea na msanii huyo aliyemwita mtoto.

"Usije ukatembea na huyo mtoto utajivunjia heshima japo huchaguagi," aliandika shabiki huyo.

Kisha yeye alimjibu "Umechelewa sana kuniambia sasa itakuwaje".

Jibu hilo lilionekana kuwashangaza wengi na baadhi walihoji itakuwaje mrembo huyo kupenda watoto kama ilivyokuwa kwa mume wake wa zamani Dogo Janja.




## INSTA-TWITTER

e-
ni
pa
mengi
ku-
am-
kila
habiki
020
u kwa



Tuffollow/ Tu-tag
@burudanitele



**Tusisahau** kuwakumbuka wazee wetu, wagonjwa, wasiojiweza na wale wenye kuhitaji msaada wetu katika kipindi hiki-**Jenifer Kyaka Odama.**



**Haikuwa** rahisi kuumaliza mwaka 2019, bali kwa neema ya Mungu tu. Tusiingie mwaka mpya 2020 na mizigo ya vinyongo, visasi, roho ya kutosamehe na wivu Ndani ya Mwaka Mpya 2020, tuuanza mwaka mpya 2020 tukiwa na moyo mweupe. Wasamehe wote waliokukosea mwaka 2019-**Riyama Ally.**



**Wakati** nwingine makosa ndio mwalimu bora na wa daraja la juu kabisa kumfunza mtu. Matokeo ya makosa ya mtu fulani huishi kichwani kwake kama funzo. Haitahitajika mtu mwingine tena kukwambia-**Yusuph Mlela.**

Kuumbe!



WAREMBO ZAIDI AFRIKA

# Jokate, Jacqueline Mengi waongoza

WAREMBO kutoka Tanzania wametamba kwa kushika nafasi za kwanza katika orodha ya wanawake wenye mvuto Afrika.

Kulingana na mtandao wa masuala ya mitindo na urembo wa nchini Nigeria umetoa orodha hiyo na kuwataja Jacqueline Mengi na Jokate Mwegelo, kuwa wanawake wenye mvuto na wenye mafanikio.

Katika orodha hiyo yupo, mshiriki wa Miss Tanzania mwaka 2000, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo.

Watanzania hao pamoja na kusifiwa kwa urembo, pia wameelezwa kuwa wamepata mafanikio katika ujasiriamali mbalimbali ambao unawapa pesa nyingi.

Jacqueline, ambaye anamiliki biashara ya samani za nyumbani, ametajwa kutokana na kutoa misaada kwa ajili ya watoto wadogo wa shule za msingi kupitia taasisi yake ya Dr. Ntuyabaliwe Foundation.

Taasisi hiyo imekuwa na mchango mkubwa wa kujenga maktaba za watoto pamoja na vifaa mbalimbali vya shule pamoja na kukarabati miundombinu ya shule.

Pia katika listi hiyo, DC Jokate ambaye ameonekana akipambana katika harakati ya kumkomboa mtoto wa kike kupitia elimu,

ametajwa kutokana na kujishughulisha kwake na biashara ya samani za majumbani kupitia brand yake ya Molocaho ambapo kwa sasa inafanya vizuri Afrika Mashariki na Afrika.





GEORGE NA WILSON



KING KIKI



# Nyimbo 5 za kukaribisha mwaka mpya

**Na Adam Fungamwango**

KAMA tulivyoendelea kusema na kuandika, muziki wa dansi ndiyo muziki pekee ambao hauachi kitu chochote kwenye jamii bila kutungia wimbo.

Unapotokea msiba, asilimia kubwa ya nyimbo zenye maudhui ya aina hiyo unakuwa ni muziki wa dansi. Yakitokea maafa yoyote nchini, nyimbo nyingi za maombolezo huwa ni za dansi na hata sikukuu za kiserikali mara nyingi, nyimbo kama za Muungano, Uhuru wa Tanganyika (sasa Tanzania Bara) huwa ni za muziki wa dansi.

Zikija sikukuu za kidini iwe Idd El Fitri au Krismasi, nyimbo zinazotamba ni za muziki wa dansi tu. Hata mwaka mpya pia, huwezi kukuta ngoma za bongo fleva zikizungumzia mambo ya mwaka mpya.

Tayari tumeingia mwaka mpya wa 2020. Kwa miaka mingi wanamuziki wa dansi wameendelea kuonyesha kuwa walikuwa bora zaidi, kwani wanazo nyimbo zinazozungumzia sikukuu ya mwaka mpya.

**SIKUKUU IMEFIKA - GEORGE PETER**

Ni wimbo ambao hutamba sana wakati wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya. Wimbo huu imetungwa na George Peter akiwa na bendi yake ya Jobiso, baada ya kutengana na kaka yake Wilson Peter Kinyonga kwa muda mfupi kabla ya kurejea tena Simba Wanyika.

Huu ndiyo wimbo maarufu zaidi wa Jobiso na baadhi ya watu hudhani ni wa Simba Wanyika.

Maudhui wa wimbo huu yanasema kuwa sikukuu za Krismasi imefika na mwaka mpya unafika, hivyo watu wote wapite salama.

Mtunzi anamuomba Mungu awalinde wote waliobaki, kwani wakati sikukuu hizo zinafika wengine wako hospitali, wapo waliofungwa na wengine wamekufa, hivyo anamuomba waliobaki wote Mungu awasaidie uzima na afya.

**TUFURAHI MWAKA MPYA - HAMZA KALALA**

NI wimbo ambao Hamza Kalala anawahimiza watu wote wafurahi na mwaka mpya, wale vizuri, wavae nguo mpya, wanywe soda na kucheza.

Anasema siku hizi kumaliza mwaka ni kazi ngumu kwa sababu ya matatizo na magonjwa mbalimbali yanayowakabili wanadamu.

Hata hivyo ukiusikiliza sana wimbo huu, Kalala amechukua maneno mengi kutoka kwa wimbo wenye maudhui hayo hayo ya 'Tufurahi Kumwaka Mpya' ambao awali ulipigwa kwenye miaka ya '50 na Jean Mwenda Bosco.

**CHRISTMAS, NEW YEAR-MBARAKA MWINSHEHE**

Mbaraka Mwinshehe alitunga wimbo wa sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya, akiwataka watu waende kwanza makanisani wakasali, lakini wakitoka huko wapitie kwenye muziki wa Volcano ambayo ni bendi aliyokuwa akiiongoza.

**CHRISTMAS, BONANE-KING KIKI**

Ni wimbo maarufu sana nchini Tanzania, hasa kinapokaribia kipindi cha sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.

"Natoka wapi, tukacheze mchezo wa sasa Kamanyola oo, tutoke naye, nakuchukua wangu kipenzi mi waoo hoho.." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo yakiimbwa na Kikumbi Mwanza Mpango King Kiki.

"Ooo Bonane mama" Ni kiitikio cha wimbo huo, wakiwa na maana mwaka mpya.

**KRISMASI NA MWAKA MPYA-MK GROUP**

Kwenye miaka ya 90, bendi matata ilivyovuma kwa kipindi kifupi lakini ikitikisa anga la muziki wa Tanzania, MK Group wakiwa na Kasongo Mpinda, walitunga wimbo wa Krismasi na Mwaka Mpya ambao nao pia ulikuwa ni moja na nyimbo maarufu sana kipindi hiki.

## IMETOKEA

# Mwizi aiba majivu ya marehemu, ajuta

NI tukio la kustaajabisha, kwani majivu ya kijana mmoja yaliyoibiwa ndani ya gari la familia yake, yamerudishwa, baada ya mtu aliyeiba kuwapigia simu huku akilia.

Familia ya Dennis Bebnarz, imesema walipanga kumwaga mabaki ya marehemu mtoto wao Dennis (pichani chini), katika sehemu yenye utulivu na nzuri baada ya kifo chake.

Walichagua kumwaga nchini, Cyprus, lakini sanduku lenye majivu yake liliibiwa nyuma ya gari lao, wakati wenyewe walipoenda kula chakula katika mgahawa.

Mama yake Dennis, Kinga Bebnarza, amesema mwizi huyo alimpigia simu akiwa analia na kuomba msamaha kwa kitendo alichokifanya.

Vilevile alimwelekeza sehemu ambayo polisi waliweza kukuta majivu hayo.

Sanduku la mbao lililotumika kuhifadhi majivu hayo lilikuwa ndani ya begi la mgongoni, liliibiwa kutoka kwenye gari la familia ya Bebnarz wakati wakiwa wanakula chakula cha mchana katika mgahawa mmoja.

Bwana na bibi Bebnarz, wanaotoka nchini Poland, lakini kwa sasa wanaishi Sweden, walisafiri kuelekea Cyprus kuyamwaga majivu ya Dennis.

Wamesema wameshindwa kusherehekea sikukuu ya Krismasi, bila mtoto wao, ambaye alifariki dunia katika ajali ya gari miezi mitano iliyopita.

"Tulitaka kwenda sehemu tulivu kufunga mwaka ambao umekuwa sio mzuri kwetu." Bi Bebnarz aliiambia BBC.

Siku ya Jumapili wanandoa walisafiri kuelekea nchini Poland baada ya kukosa matumaini ya kuyamwaga majivu ya mtoto wao.

Bi. Bebnarz amesema ameuacha moyo wake nchini Cyprus, huku akihofia kuwa majivu ya mwanae yametupwa kwenye shimo la takataka au sehemu mbaya zaidi.

Wazazi hao waliamua kutumia vyombo vya habari kuwaomba wezi au mwizi kurudisha majivu ya mtoto wao.

Lakini jambo ambalo lilimshangaza sana ni pale alipopokea simu ya mtu anayedhaniwa kuwa ni mwizi wa majivu hayo siku ya Jumapili akiwa analia.

Alisikika akiomba msamaha mara kwa mara na kumwambia sehemu wanayoweza kukuta sanduku hilo lenye majivu na kuwaataarifu polisi ambao waliweza kulifuatilia na kulikuta karibu na barabara.

Sanduku hilo lilikuwa limeandikwa jina la Dennis likiwa na mwaka wake wa kuzaliwa na wa kufariki dunia. Alizaliwa mwaka 2000 na alifariki 2019.

Polisi wamethibitisha kuwa raia watatu wa Cyprus wamekamatwa juu ya wizi huo.

Wanaume wawili na mwanamke mmoja wanakabiliwa na mashtaka yanayohusu ya kuharibu na kuiba kutoka kwenye gari.


Bi. Bebnarza aliiambia BBC kuwa hana kinyongo na mwizi huyo, lakini anatumaini kuwa atabadilisha maisha yake.

"Ana hisia za mwanadamu na moyo mzuri sana," alielezea.


"Kuna mwisho mzuri" aliongeza hayo licha ya hali mbaya wanayopitia sasa wazazi hao.

Watasafiri kuelekea Cyprus baada ya kuchukua majivu ya Dennis. "Tunahitaji kutuliza hisia zetu kwanza" amesema Bebnarz. "Sijalala tangu Ijumaa."

Lakini amesema sasa wanajisikia wamekamilika baada ya kurudishiwa majivu ya mtoto wao.








# Ukurasa Mpya Mapenzi hayana mbwembwe

**Na Adam Fungamwango**

KUNA watu hudhani kuwa wanapendwa kwa sababu ya ustaa wao. Wengine wanaamini wanapendwa kwa pesa walizonazo, urembo, uzuri au utajiri.

Wasichokijua ni kwamba mapenzi huwa hayafananishwi na kitu chochote kile. Mapenzi hayana fomula, yaani mbili jumlisha mbili ni lazima iwe nne.

Ni kwamba mtu anatokea tu kupenda na hata wenyewe haswa hajui ni kwa nini anapenda. Hutokea tu bila sababu yoyote inayoonekana au kusimulia.

Ni sababu ambayo imo ndani ya moyo wa mtu mwenyewe na ina nguvu ambayo inamvuta na kumlazimisha mwenyewe bila kujijua nini anafanya.

Ndiyo maana wapo wanaosema anayependa haoni wala hasikii. Kwenye pengo huona kuna mwanya na kwenye chongo huona kuna kengeza.

Ukitaka kuthibitisha hili hebu fuatilia filamu hii iitwayo 'Ukurasa Mpya'.

Imechezwa na Jacob Steven maarufu kama JB, Halima Yahaya, Eshe Buheti, Banana Zorro, Soud Ally, Hussein Njenje na wengineo. JB ana rafiki zake ambao ni Zanana na Soud. Hawa ni vijana zaidi, hivyo humtegemea zaidi JB kuwapa nasaha za maisha na hata za kikazi.

Hii inawafanya wafanikiwe. Wanafanikiwa kazini. Wanafanikiwa kuwapata wapenzi ambao wanawafanya kuwa na furaha.

Hata hivyo, hali ni tofauti kwa mwalimu mwenyewe. Yeye anakimbiwa na mpenzi wake Halima. Sababu kubwa ni kwamba, JB ni Mwandishi wa Habari.

Kutokana na kazi yake hasna muda wa kukaa na familia yake, badala yake yeye kazi, kazi na yeye.

Hali hii inamfanya Halima kuwa mpweke. Na katika kuondokana na hali hiyo, anampata mwanaume mwingine.

Hii inamuumiza sana JB na kumkosesha raha na amani moyoni. Rafiki zake nao kutokana na mtu wao kuwa kwenye hali hiyo, nao walikosa raha.

Mtu wanayemtegemea kuwapa michongo ya kazi na mapenzi, akili zake zimevurugika kutokana na mapenzi.

Wakakaa kikao na kupanga mikakati ya kufanya ili kumrudisha mwalimu wao kwenye furaha waendelee kuvuna ujanja, hekina na busara zake.

Kwanza kabisa walichogundua ni kwamba rafiki yao hawezi kuwa na furaha akiwa na mwanamke yoyote yule zaidi ya Halima tu.

Banana anajifanya ni mtu anayefanya kazi ya kupuliza dawa ya kuuliza wadudu, hivyo akajipenyeza na kupata kazi kwenye kwa kina Halima.

Soud yeye akajigeuza kuwa mhudumu wa baa na kupata kazi jirani kwa kina Halima. Halima yeye kila anapopata nafasi anakwenda kunywa kwenye baa hiyo ambayo mhudumu wake ni Soud.

Siku isiyo na jina, Halima na mchumba wake kwenye baa hiyo anayofanya kazi Soud, JB akiwa amejificha sehemu na Banana.

Waliingia kwa mikogo, lakini kwa ufundi wa hali ya juu Soud alijifanya amejikwaa na kumwagia kinywaji mchumba wa Halima. Kukatokea kutoelewana, lakini kwa bahati nzuri Halima alimtambua Soud na kumwambia mchumba wake atulie kwani ni jambo dogo tu, hivyo aende msalani kujisafisha.Wakati jamaa yuko msalani, JB alitumia muda huo kufuata Halima na kukiri kosa lake, akiahidi hatorudia tena.

Hivyo ndivyo JB na Halima walivyomaliza tofauti zao, Soud na Banana wakafurahi mwalimu wao kurudisha furaha yake.



## MAJUTO 2020

# Yamkuta, apata hofu ya ndoa yake

MWAKA 2020 umeanza vibaya kwa mwanamuziki nyota wa Nigeria, Davido, ambaye hivi sasa anajitahidi kunusuru kuvunjika kwa mipango yake ya harusi.

Juzi tu, Davido, alionekana kumjali mchumba wake, Chioma, kiasi ambacho walionekana kila kona ya Dubai wakila bata na mtoto wao mchanga.

Hata hivyo, safari yake ya kwenda nchini Ghana kwa ajili ya kutumbuiza, imempaka matope na sasa anaamua kujiosha kunusuru ndoa yake isiyeyuke kama barafu.

Tukio lenyewe lilikuwa hivi! Davido alipokwenda nchini humo, aliambatana na mpenzi wake wa zamani ambaye amezaa naye mtoto mmoja.

Wakiwa kwenye ndege, wawili hao waliposti picha mbalimbali na kuzitupia kwenye mitandao ya kijamii.

Lakini mashabiki hawakupendezwa nazo, badala yake walimshambulia kwamba kitendo hicho kinamvunjia hadhi mkewe mtarajiwa, Chioma, na kwamba hakifai kufanywa na staa mkubwa kama yeye.

Mambo yalivyozidi kuwa mabaya, Davido, sasa ameibuka na kukana tuhuma zinazodai alikuwa akila bata na mwanamke aliyezaa naye.

Mwanamuziki huyo, amejitetea kwamba hakuwa safari moja na mama wa mtoto wake wakati akienda Ghana, badala yake mwanamke huyo alimpatia lifti ya kwenda huko kwa ajili ya biashara zinazomuhusu mtoto wao.

Davido ametoa ufafanuzi huo baada ya watu kumshtumu kwenye mitandao ya kijamii, ambapo yeye ameeleza kuwa hajapendezwa na suala hilo, kwani linamvunjia heshima mchumba wake Chioma pamoja na familia yake.

Amesema tuhuma hizo zinaweza kuvunja malengo yao ya kuingia kwenye ndoa hivi karibuni.

Kupitia Instastory yake Davido ameandika, "Nyie wote mnafahamu kuwa nimeshamchumbia mpenzi wangu Chioma, haitakuwa na maana kwa mimi kufanya hivyo mnavyosema, mama wa mtoto wangu alikuwa na bishara ya bidhaa za nywele Ghana, na mimi hivyo hivyo nilikuwa nimealikwa kuburudisha kwenye Afronation, hivyo nikampa lifti mpaka Ghana."

Akaongeza "Sijaelewa kwanini mnasambaza taarifa za uongo, mnajua hazitafanya kitu ila zimeniumiza na kuishushia heshima familia yake, 2020 ni kwa ajili ya mambo chanya tu."

# Davido afurahia kumshika Rais wa Ghana



KATIKA mambo ambayo atayakumbuka mwanamuziki Davido mwaka 2019, ni tukio la kukaa pamoja na Rais wa Ghana na mkewe.

Davido alishirikisha video fupi, akionekana yupo pamoja na kiongozi wa nchi hiyo Nana Akufo-Addo, na mkewe Rebecca Akufo-Addo.

Mkali huyo alikuwa Ghana kwa ajili ya kutumbuiza mkesha wa mwaka mpya na hapo ndipo alipofanikiwa kukaa na kiongozi huyo.

"Naipenda Ghana," aliandika Davido chini ya video hiyo.



## Mchumba wa Bobby Kristina Brown naye afariki

MCHUMBA wa zamani wa Bobbi Kristina Brown, Nicki Gordon amefariki dunia baada ya kuzidiwa na dawa za kulevya.

Nick Gordon (30), mchumba wa zamani wa binti wa mwanamuziki Whitney Houston, Bobbi Kristina Brown ambao wote walikufa kutokana na matumizi ya dawa za kulevya, amekufa kwa kile kinachodaiwa kuzidisha kiwango cha dawa za kulevya.

Kulingana na mtandao wa PageSix, Nick Gordon, 30, alipatwa na shambulio la moyo baada ya kutumia kiasi kikubwa cha dawa hizo, alifariki akiwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Altamonte Springs.

## DJ Cuppy aanza mwaka akiwa singo

MMOJA wa waburudishaji maarufu nchini Nigeria, DJ Cuppy, ameweka wazi kwamba mwaka huu umeanza akiwa singo.

Akitupia ujumbe katika akaunti yake ya 'Instagram stories on Thursday', amesema alipata hofu kuingia mwaka mwingine akiwa hana mpenzi na inafaa kubadili jina.

"Nimejaribu nitabadili vipi jina mwaka 2020, bado nipo singo," aliandika DH Cuppy.





## Omotola atuliza hali ya hewa

MWIGIZAJI mkongwe Nigeria, Omotola Jalade-Ekeinde, ameamua kusafisha hali ya hewa baada ya kutangaza hana ugomvi na msanii mwenzake Genevieve Nnaji.

Katika akaunti yake ya Twitter, Omotola aliwaambia wafuasi wake kwamba uvumi unaonea kwamba yeye na staa mwenzake Nnanji wana ugomvi wa siku nyingi ni uongo mtupu na wakati wote wanasalimiana.

"Napenda kuangalia picha zako @GenevieveNnaji1. Hii itakuwa nafasi njema kukutakia mema baada ya fununu kwamba mastaa wawili wakubwa wanawake wa filamu kuwa ni maadui wakubwa," aliandika Omotola kwenye Twitter.

## 2Baba apewa ufalme wa muziki


MKONGWE wa muziki toka Nigeria, 2baba, ameweka historia nyingine baada ya kufanya vizuri katika kubwa la '20years a king concert', ambalo lilifanyika wiki iliyopita.

2baba ambaye ni mfalme wa uimbaji aliwapagawisha mashabiki wake kwa nyimbo nyimbo zake, alipanda jukwaani sambamba na msanii mwenzake Wizkid.

Katika tamasha hilo wasanii mbalimbali walitumbuza wakiwamo Patoranking, Terry G, Solidstar, Reekado Banks, 9ice, Ycee, Waje na wengine.



## SAFU



**KALAMU YA MWALIMU**

# Waajiri wanaotoa taarifa za uongo wanavunja moyo watumishi kiutendaji

**Na Reubeni Lumbagala**

KHERI ya Mwaka Mpya wa 2020 ndugu msomaji wa Safu hii ya "Kalamu ya Mwalimu".

Baada ya mapumziko mafupi, nimerejea tena katika kuhabarishana na kuelimishana masuala mbalimbali ya elimu na maendeleo ya jamii.

Ikiwa leo ni siku ya nne tangu tuuanze mwaka mpya wa 2020, Kalamu ya Mwalimu inaanza mwaka huu kwa kujadili suala la udanganyifu linalofanywa na waajiri wasio waadilifu na waaminifu ambao hutuma taarifa za uongo kwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuwezesha watumishi wasio na sifa kupanda vyeo au madaraja.

Kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya utumishi wa umma, watumishi wa umma wanayo haki ya kupandishwa vyeo au madaraja.

Baada ya mtumishi wa umma kukidhi vigezo vya kupanda cheo au daraja, mwajiri wake anao wajibu wa kutuma taarifa muhimu za mtumishi wake kwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili aweze kupata haki yake ya kupanda cheo au daraja kutokana na utendaji kazi uliotukuka pamoja na kuchangia mafanikio katika taasisi anayofanya kazi.

Kila mtumishi wa umma anatamani apande cheo au daraja kwani jambo hili linachangia ongezeko katika mshahara wake na kumwongezea sifa katika utendajikazi. Lakini ifahamike kuwa suala la kupandisha vyeo au madaraja watumishi wa umma linafanywa kwa kufuata sheria na kanuni za Utumishi wa Umma na si jambo linalofanywa kiholela na kwa utashi binafsi wa mwajiri.

Hivyo basi, linapokuja suala la waajiri kutuma taarifa za watumishi wao wanaostahili kupanda vyeo au madaraja, ni lazima waajiri wazingatie sheria na kanuni na watume taarifa za watumishi wale tu waliokidhi sifa za kupanda vyeo na si vinginevyo.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Laurean Ndumbaro, akizungumza na waandishi wa habari juma lililopita, alizungumzia namna serikali ilivyojipanga kuajiri watumishi 40,000 wa kada mbalimbali mwezi Februari, 2020. Pamoja na nia njema hii ya serikali, Dk. Ndumbaro alizungumzia pia namna ofisi yake ilivyobaini baadhi ya waajiri wasio waaminifu wanaowasilisha taarifa za uongo za watumishi wao ili kuwezesha kupanda vyeo kinyume kabisa na sheria na kanuni za utumishi.

Jambo hili ni baya ambalo linapaswa kulaaniwa vikali na kila mpenda haki na maendeleo ya Utumishi wa Umma kwani kwa kufanya hivi watumishi wa umma wanavunjika moyo katika utendajikazi wao wa kila siku.

Ni dhahiri shahiri kuwa waajiri na wakuu wa taasisi wanaowasilisha taarifa za uongo wanawanyima haki watumishi wengine ambao wana haki ya kupanda vyeo au madaraja. Pia suala hili linachangia ongezeko la rushwa katika maeneo ya kazi.

Na hii inapelekea ufanisi wa kazi kupungua kwani watumishi watajikita katika kutafuta fedha kwa ajili ya kutoa rushwa ili waweze kupanda vyeo na si kujituma kazini kama sifa ya msingi ya kupanda cheo.

Tupo katika Awamu ya Tano ambayo inasisitiza watumishi wake kuacha kufanya kazi kwa mazoea ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Utendajikazi wa mazoea uliogubikwa na vitendo vya rushwa ni kikwazo kikubwa cha mafanikio.

Aidha, mikakati na mipango mingi iliyowekwa na serikali haiwezi kufanikiwa kwa utendajikazi wa mazoea usio na tija na ndiyo maana uchapakazi uliochanganyika na uaminifu na uadilifu unasisitizwa sana kwa viongozi, watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla ili kuchagiza kasi ya maendeleo.

Kalamu ya Mwalimu inaungana na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma kulaani baadhi ya waajiri wanaofanya uhuni wa kuwasilisha taarifa za uongo, ili kutoa upendeleo kwa watumishi ambao hawajakidhi vigezo vya kupanda vyeo au madaraja.

Waajiri wanaofanya hivi wanapaswa kuacha mara moja tabia hii kwani inawavunja moyo watumishi wa umma wenye moyo wa uwajibikaji na uchapakazi.

Wakati huu ambao serikali imejipambanua pasi na shaka kuwa utendaji kazi uliotukuka ndiyo msingi wa kupanda cheo au daraja, ni lazima suala hili likasimamiwa ipasavyo ili kuongeza tija katika maeneo ya kazi.

Vilevile, waajiri wawatendee haki watumishi wao kwa kuwapa haki zao pasipo kuwaomba rushwa ili kuwawezesha kupanda cheo. Miongoni mwa majukumu ya waajiri ni pamoja na kushughulikia taarifa za watumishi wao ili kuwawezesha kupata haki zao. Hivyo, waajiri wawasilishe taarifa za watumishi wao kwa wakati kwa kuzingatia sheria na kanuni za utumishi na si vinginevyo.

Pia, adhabu sahihi kwa waajiri wanaoendekeza vitendo vya rushwa kwa kuwasilisha taarifa za uongo ili kutoa upendeleo wa watumishi wanapaswa kufukuzwa kazi mara moja ili kuwa fundisho kwa wengine.

**Tafakari.**

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Maoni: (+255) 764 666349.**

# 2020 mwaka wa uchaguzi Afrika Mashariki

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 2020 imeelezwa kuwa wa mitikisiko ya kiasiasa kutokana na nchi nne kuwa katika matayarisho ya uchaguzi mkuu.

Kutokana na umuhimu wa ratiba yake utakuwa na matukio makubwa ambayo yatakuwa sehemu ya historia na kukumbukwa kwa miaka mingi ijayo.

Nchi za ukanda wa Afrika Mashariki ambazo mwaka huu zitakuwa katika matukio makubwa ya chaguzi za kuwachagua viongozi wa ngazi za juu serikalini ni Tanzania, Burundi, Uganda na Ethiopia.

**BURUNDI KUAMUA**

Mei 20 mwaka huu, Warundi watakuwa wanapiga kura ya kumchagua rais wao baada ya Pierre Nkurunziza (pichani), kumaliza muhula wake wa madarakani.

Hata hivyo, kuna jambo ambalo linasubiriwa kwa hamu, nalo ni kuona kama Rais Nkurunziza ataamua kung'atuka au kuendelea kugombea nafasi yake.

Tangu mwaka 2015, Burundi imekumbwa na machafuko ya kisiasa ambayo yamegharimu maisha ya mamia ya watu, maelfu wengine kwenda ukimbizini.

Chanzo cha machafuko ilikuwa ni tofauti za tafsiri ya katiba na hatimaye Nkurunziza kuongeza muhula wa tatu madarakani.



Mwaka 2018, Burundi ikaandaa kura ya maoni ambayo ilibadili katiba na kurefusha mihula ya urais madarakani kutoka miaka mitano hadi saba. Hatua hiyo ikatafsiriwa na wengi kuwa ni maandalizi ya Nkurunziza kusalia madarakani baada ya 2020. Vyama vya upinzani na makundi ya wanaharakati vimekuwa vikipinga hatua hiyo. Vyombo vya habari vya ndani na nje vimekumbana na mkono wa dola. Mashirika ya habari ya kimataifa kama BBC na VOA yamepigwa marufuku nchini humo.

**TANZANIA KUMEKUCHA**

Huu ni mwaka wa uchaguzi nchini Tanzania, muhula wa kwanza wa Rais John Pombe Magufuli, unafikia tamati Oktoba 2020.

Kwa utamaduni wa chama tawala Tanzania cha CCM, Rais anayemaliza muhula wa kwanza hupitishwa bila kupingwa kwenda kugombea muhula wa pili na wa mwisho wa urais wa nchi.

Hata hivyo, kuna fununu kuwa baadhi ya makada waandamizi wa chama hicho ambao wanapanga kumpinga Magufuli katika kuwania awamu ya pili ya urais ndani ya CCM.

Jina la Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje wa Tanzania, Bernard Membe, limekuwa likitajwa katika fununu hizo, hata hivyo mwenyewe hajazungumzia jambo hilo kama ni kweli.

Kwa upande wa upinzani, mambo kwao yamezidi kuwa magumu kutokana na muungano wao kuyumba na baadhi yao kuhamia chama tawala.

Baadhi ya wabunge wa upinzani na madiwani wamevihama vyama vyao na kuelekea CCM katika kile kilichoitwa kuunga mkono juhudi za maendeleo za Rais Magufuli.

Mwishoni mwa mwaka jana, ulifanyika uchaguzi wa serikali za mitaa nchini humo. Vyama vikuu vya upinzani vilisusia uchaguzi huo vikilia kuchezewa rafu. Mwishowe 'CCM ilishinda kwa kishindo.

Kwa upande wa visiwa vya Zanzibar, Rais Ali Mohammed Shein anamaliza miaka yake 10 na hivyo kutoa nafasi kwa mtu mwingine kuongoza nchi hiyo.

**ETHIOPIA MAJARIBU TENA**

Tangu kuingia madarakani, Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, mambo yamebadilika kwa kasi nchini humo.

Ethiopia ambayo ilikuwa na jina baya la kuminywa kwa demokrasia, maandamano ya upinzani wa jamii ya Waoromo na mgogoro wa mpaka baina yake na Eritrea, lakini yote hayo yamepatiwa ufumbuzi.

Wafungwa wa kisiasa wameachiwa, maandamano yameisha, na Baraza la Mawaziri likapata uwakilishi mkubwa wa wanawake.

Yote hayo yamefanywa na Waziri Mkuu kijana Ahmed ambaye kwa sasa ana miaka 43.

Ahmed kwa kipindi hiko kifupi amefanikiwa kushinda tuzo ya amani ya Nobel.

Mambo hayo yakitokea, si kila mtu ambaye alikuwa akiridhishwa na kinachoendelea, jaribio la mapinduzi dhidi ya Abiy lilifanyika na kushindikana, tukio hilo lilisababisha mkuu wa majeshi kuuawa.

Ethiopia itafanya uchaguzi mkuu mwezi Mei 2020, huku ikionekana kama umaarufu na ushawishi wa Ahmed ukifunika wapinzani wake.

**BBC**

MAKALA

# NEC NA UTOAJI WA ELIMU YA MPIGAKURA ANA KWA ANA KUHUSU UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGAKURA YAWAFIKIA MAKUNDI YOTE



Ofisa wa NEC, Meshack Mgovano, akiwa katika utoaji wa elimu ya mpigakura kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura iliyofanyika katika Shule ya Sekondari Mwl.Nyerere Mjini Tunduma Mkosni Songwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Christina Njovu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inaendelea na zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura ambalo ni mahsusi kwa ajili ya kuandikisha wapigakura wapya wenye sifa ya kuwamo katika Daftari la Kudumu la Wapakura na hatimaye kupiga kura.

Miongoni mwa sifa hizo, ni pamoja na waliotimiza umri wa miaka 18 na kuendelea ambao hawakuwahi kujiandikisha hapo awali na wale ambao watatimiza umri wa miaka 18 ifikapo siku ya Uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka 2020 vijana hawa ni wale walizaliwa mwaka 2002 kuanzia Januari hadi Oktoba, awe ni raia wa Tanzania, pia ni mtu mwenye akili timamu.

Kinachoenda sambamba na utoaji wa elimu ya mpigakura kwa njia ya gari la matangazo ikiwa ni moja ya michakato muhimu kuelekea uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani utakaofanyika mwaka ujao wa 2020.

Utoaji wa elimu ya mpigakura unaofanyika hivi sasa ni kwa ajili ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ambao unawaelimisha, kuwafahamisha na kuwajulisha wananchi juu ya sifa za mtu kujiandikisha kuwa mpigakura ili kupata kadi ya kupigia kura ambayo ndio atakayoitumia kupiga kura siku ya uchaguzi mkuu ujao na chaguzi ndogo zitakazojitokeza.

Uboreshaji huo ambao unafanyika kikanda elimu ya mpigakura nayo inaendelea kutolewa kulingana na mwenendo mzima wa zoezi kukiwapo gari la matangazo linapita katika baadhi ya mikoa, miji na viunga vyake zikiwamo shule za sekondari ambako ndiko kuna wapigakura wapya kwa lengo la utoaji elimu ya mpigakura juu ya umuhimu wa kujiandikisha.

Kwa kutumia njia hiyo ya utoaji wa elimu ya mpigakura kwa njia ya gari la matangazo, Tume imeweza kuwafikia wananchi walio wengi, makundi mbalimbali yakiwamo makundi maalumu na hasa vijana ambao ni wapigakura wapya hasa katika maeneo ya shule za sekondari, maeneo yenye mikusanyiko ya watu ya ikiwamo masoko, stendi na magulio.

Moja ya malengo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni kuwafikia wapigakura wapya ambao wengi wao ni vijana ambao wametimiza umri wa miaka 18 ambayo ni miongoni mwa sifa kuu ambayo inamwezesha mtu kuwa mpigakura zikifuatiwa na kuwa raia wa Tanzania pamoja na kuwa na akili timamu.

Sambamba na hilo, mtu atakosa sifa za kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura ikiwa ni raia wa nchi nyingine, imethibitika na daktari kuwa hana akili timamu, yuko kizuizini kutokana na uhalifu kwa maana ya kuwa amefungwa jela, akiwa amehukumiwa adhabu ya kifo, ikiwa anatumikia adhabu ya kifungo kinachozidi miezi sita kilichotolewa na mahakama na kama amepoteza sifa za kuwa Mtanzania kwa mujibu wa sheria za uchaguzi au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge.

Katika shule mbalimbali za sekondari ambayo Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kutumia gari la matangazo limeweza kupita wanafunzi waliweza kupata elimu sahihi ambayo iliwaimarisha katika somo la uraia na waliweza kuuliza maswali na kujibiwa papo kwa papo na hatimaye kukuza uelewa wao.

Mmoja wa walimu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mpanda (Mpanda Girls) ameishukuru Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuweza kuchagua shule yake kuwa moja ya shule ambayo imetembelewa na Tume na kupatiwa elimu ya mpigakura na kwamba elimu hiyo ni miongoni mwa elimu inayotolewa katika somo la General Study (GS).

Baadhi ya wanafunzi katika shule zilizopatiwa elimu hiyo na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutoa elimu ya mpigakura shuleni na kueleza kuwa elimu hiyo imewasaidia kujua sifa za mtu kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura sambamba na sifa za kuwa mpigakura, alisema Agnes Kilangi wa Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Maurusia niliyopo Sumbawanga mkoani Rukwa.

Elimu ya mpigakura inayotolewa na Tume kwa njia ya gari la matangazo imewazesha wananchi kupata uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya uchaguzi, ambapo wamekuwa wakiuliza maswali mbalimbali na kujibiwa na maofisa wa Tume, wamepatiwa pia vipeperushi vinavyowasaidia kuelewa zaidi mchakato mzima wa uchaguzi.

Mikoa ambayo gari la tume imepita ni pamoja na Mkoa wa Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Simiyu katika viwanja vya Nyakabindi wakati wa Maonyesho ya Nanenane, Mara, Geita, Mwanza, Bukoba, Tabora, katavi, Rukwa, Mbeya, Dodoma na hivi sasa lipo mkoani Iringa likiendelea na zoezi zima la utoaji wa elimu ya mpigakura kupitia maofisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Gari la matangazo liliweza kupita katika mikoa hiyo na kutoa elimu ya mpigakura katika maeneo mbalimbali yenye mkusanyiko wa watu, sambamba na katika maonesho ya Nanenane yaliyofanyika kitaifa mkoani Simiyu katika viwanja vya Nyakabindi, stendi na katika maeneo ya masoko na kutoa fursa kwa wananchi kuuliza maswali na kujibiwa papo kwa papo.

Sambamba na utoajia elimu ya mpigakura kwa njia ya gari la matangazo uwafikia wapiga kura anakiwa na pia elimu hiyo inatolewa kwa njia ya redio za kijamii zinazopatikana katika mikoa yote ambao maofisa wa Tume ya Uchaguzi wamekuwa wakizungumza na wananchi na kujibu sambamba na kutoa ufafanuzi katika masuala mbalimbali ya Uboreshaji na Uchaguzi kwa ujumla.

Hivyo, wananchi tutumie fursa hii adhimu tunapoliona gari la matangazo la Tume ya Uchaguzi, tusogee na tutege sikio kusikiliza elimu inayotolewa na Tume.

Kadi yako Kura yako Nenda Ukajiandikishe

MAKALA

# Musoma vijijini yajizatiti kilimo

## ■Wakulima wapewa bure plau kuongeza uzalishaji

Na Sabato Kasika

SERIKALI imeweka mkakati maalum wa kuhakikisha inamkomboa mkulima anaondokana na matumizi ya jembe la mkono na badala yake kutumia zana za kilimo.

Lengo kubwa la mkakati huo ni kumfanya mkulima kutoka kwenye kilimo cha kujikimu na kuwa cha kibiashara ili kujiinua kiuchumi.

Hii ni kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, ambaye anasema asilimia kubwa ya wakulima nchini wanatumia majembe ya mkono.

Ndivyo waziri huyo alikaririwa na vyombo vya habari Septemba mwaka jana, na kueleza kuwa mbali na jembe la mkono, pia kilimo kinategemea msimu wa mvua jambo ambalo ni vigumu kuondokana na umaskini.

"Tunatumia majembe ya mkono, mbaya zaidi kilimo chetu kinategemea msimu wa mvua, hivyo kilimo cha aina hii bado kinatuchelewesha, tuna wajibu wa kujifunza kwa wenzetu walioendelea," anasema Hasunga.

Hasunga anasema, kwa kuanza, serikali kwa kushirikiana na wadau wa kilimo itajenga mabwawa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, ili kuongeza uwezo katika uzalishaji wa mazao.

Waziri huyo anasema, kilimo cha umwagiliaji kinaweza kufanya kazi msimu mzima na uzalishaji wake unakuwa mkubwa na kumfanya mkulima kunufaika na nguvu zake.

Kwa kushirikiana na Wizara za Mifugo na Uvuzi na Viwanda na Biashara, zitafanya kazi kwa pamoja, ili kuona namna ya kuzalisha mazao ya kilimo kwa tija.

**JEMBE LA PLAU**

Utumiaji wa teknolojia katika kilimo hurahisishia kazi wakulima hasa wanawake ambao hushiriki katika kazi nyingi za shamba.

Baadhi ya zana hizo zinazohitajika zaidi kwa mwanamke ni plau, yaani jembe la kukokotwa na wanyama kazi wakiwamo ng'ombe na punda ambalo hutumiwa na baadhi ya wakulima hapa nchini.

Teknolojia hii humwezesha mkulima kufanya kazi za kilimo kwa muda mfupi na humpunguzia uzito wa kazi. Jembe la kukokotwa na wanyamakazi, lina uwezo wa kulima katika udongo mzito au mwepesi, hivyo kurahisha zaidi kilimo kuliko jembe la mkono.

Baadhi ya maeneo nchini wadau wa kilimo wameanza kampeni za kuachana na jembe hilo ili kwenda kwenye plau.

Mojawapo ya maeneo hayo ni Musoma Vijijini mkoani Mara, ambako kampeni za kuhamasisha wakulima kujikita katika jembe la kukokotwa na ng'ombe inafanyika.

Kampeni hizo zilizinduliwa Desemba 24 mwaka jana na Mbunge wa Musoma Vijijini Profesa Sospeter Muhongo, kwa kugawa plau 20 kwa vikundi 20 kutoka vijiji 20.

"Kimsingi ni kwamba tumeanza rasmi kampeni za kuhamasisha wakulima kuachana na jembe la mkono ili watumie plau na kisha baadaye wahamie kwenye trekta," Prof. Muhongo anasema.



Wakulima wa Kijiji cha Kamuguruki wakijiandaa kufunga plau kwa ajili ya kukokotwa na ng'ombe.

Anawaomba wadau wengine wa kilimo jimboni mwake kuunga mkono juhudi hizo ili wakulima wa vijiji vyote 68 wanufaike kwa matumizi ya jembe la plau.

"Tunafanya mambo yake kwa vitendo kwa ajili ya wananchi wetu, hivyo ni muhimu kuwa na kilimo chenye tija, hasa kwa kuzingatia kwamba wakulima wamehamasika kulima mazao mapya ya biashara," anasema.

Anasema, wakazi wa jimbo lake wamekuwa wakijishughulisha na kilimo cha mahindi, mpunga, mihogo, viazi vitamu, maharage, mtama, ulezi na sasa wameongeza mazao mapya ya alizeti na dengu.

**MATREKTA**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma, Charles Magoma, anasema, kuna utaratibu unaandaliwa na halmashauri yake kwa ajili ya kuvisaidia vyama vya ushirika vya msingi kupata matrekta.

Anafafanua kuwa Musoma Vijijini kuna jumla ya vyama vya ushirika vya msingi 35, na kwamba halmashauri iko tayari kusaidia kutayarisha nyaraka za kutafuta mikopo ya kununulia matrekta kwa ajili ya kilimo.

"Hizi ni kampeni za kusaidia wanachama wa vyama hivyo vya ushirika ili nao walime mashamba makubwa kwa muda mfupi na ikiwezekana wapate mazao mengi na kujiimarisha kiuchumi," anasema Magoma.

Anasema kutoka kwenye jembe la mkono na kutumia la kukokotwa na ng'ombe na pia trekta, ni mwelekeo wa kuachana na kilimo cha jembe hilo ambalo limekuwa likimtesa mkulima kwa miaka mingi.

"Mbunge ameonyesha njia na sasa wadau wengine hawana budi kuunga mkono juhudi hizo, ili ikiwezekana, jembe la mkono libaki historia tu kwamba zamani lilikuwa linatumika," anasema.

Anasema ingawa plau nayo ina matatizo yake, lakini mkulima anaweza kulima eneo kubwa kwa muda mfupi kuliko jembe la mkono, hivyo bado ni vyema itumike hiyo kuliko jembe la mkono.

"Kwa uzoefu uliopo ni kwamba, mkulima anayetumia plau anaweza kulima shamba ekari moja kwa siku moja badala ya siku tano hadi saba, ambazo hutumia kwa jembe la mkono," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, kilimo cha kutumia zana za kisasa za kilimo kinaweza kusaidia kuondokana na jembe la mkono na kuongeza tija na hivyo kuvutia vijana kwenye sekta hiyo.

Anasema, Watanzania bado hawajafikia kuwa na zana za kisasa za kilimo, lakini plau na trekta yanaweza kumsaidia mkulima kufanya kazi zake kwa rahisi na kuongeza kipato.

"Hivyo kulingana na dhana hizo, sisi tumeamua kuunga mkono juhudi za serikali ili kuhakikisha wakulima wetu wanahama kutoka hatua moja kwenda nyingine, lengo likiwa ni kuboresha kilimo chetu," anasema.



Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo (mwenye tisheti ya bluu) na baadhi ya wanachama wa vikundi vya wakuliwa, wakiwa na moja ya plau alizogawa jimboni. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 27 00)



**Dondoo: Kulia**

1. Dalili
3. Kitabu chenye maana ya maneno
6. Nia, kusudio
8. Toa makosa
10.Wingi wa n eno wimbo
13.Mwandishi katika kikao
14.Tarakimu 15. Kodi, ushuru
17. Zamani iliitwa Kazeh
20.Mpaka baina ya Kenya na Uganda 21. Ng'ata
22.Mwanamume asiye na mke
24.Binadamu
25.Bandari ya pili kwa ukubwa nchini 26. Mola
27.Mwanamke mzee 28.Saidia

**Dondoo: Chini**

1. Nchi ya nne kwa uwingi wa watu duniani
2. Fanya kwa kupenda
4. Ghasia, kero, shida
5. Chanzo cha kitu
7. Tamka maneno kimuziki
9. Makubaliano ya watu kwa maandishi
11.Mtu katili
12.Lia kukumbuka marehemu
16. Bei ya kitu
18. Ubapa
19. Chana kitu
23.fanya jambo kwa kupokezana
24.Ugonjwa wa kichwani
25. Kifaa kitoacho mwanga

## Jibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| T | A | B | I | B | U | | O | | D | | S | |
| H | | A | | | B | U | N | D | U | K | I | |
| A | S | K | A | R | I | | Y | | A | | N | |
| M | | W | | A | A | L | A | M | | O | G | A |
| A | D | A | B | U | | A | | | O | N | E | A |
| N | | T | | N | | U | M | I | Z | A | | J |
| I | | A | N | D | A | M | A | N | A | | | E |
| | P | | K | I | B | U | D | U | | U | | E |
| S | O | K | O | | I | | A | K | I | D | A | |
| | R | | M | | R | | R | A | T | I | B | A |
| M | I | G | O | D | I | | A | | I | | U | |
| | N | | | | A | | K | | K | A | D | A |
| S | I | M | B | A | | B | A | B | A | | U | |

# 2019; Mjadala elimu ulihamia ufundishaji walimu, si mitaala

**Na Michael Eneza**

BADO wataalamu hapa nchini na wenzao kutoka nje wanaendelea kujadiliana na kupeana mawazo, huku makongamano au mikutano ya kawaida ya vipindi maalum ikitafuta njia ya kujumuisha mawazo yanayotolewa kuwa mapendekezo halisi.

Tofauti ya mawazo ya mtu mmoja na mapendekezo ni kuwa inabidi wazo liwe limekubaliwa na wengi, na kuwapo utafiti wa kutosha kumwonyesha mtaalamu huyu au yule kuwa likitumika linaweza kuzaa matunda. Mawazo kama hayo hupatikana katika masuala ya mitaala kwani majaribio ni mengi, si ualimu.

Tofauti kati ya kuweka mitaala ya masomo ya shule za msingi au sekondari, na hata vyuo kwa upande huo ingawa hakuna mijadala ya wazi kuhusu mitaala ya vyuo, ni kuwa ngazi inavyozidi kupanda kijamii ndivyo tatizo linavyokuwa kubwa zaidi.



Wadau wa masomo ya shule za msingi ni walimu wa kawaida kabisa ambao hawana sauti wizarani, na katika jamii washikadau muhimu wanakuwa ni wale wenye shule binafsi, na jumuiya zinazosimamia shughuli zao. Ukija upande wa sekondari hali ni tofauti kidogo kwani mitaala yake ni mipana na ya gharama zaidi.

Unapoona mijadala inahama kutoka mitaala kwenda ufundishaji wa walimu kuna maswali kadhaa ya kujiuliza pamoja na tamati za wazi ambazo zinajitokeza kwa pendekezo hilo tu, kimantiki.

Ila kinachoendelea hakijitokezi kimantiki moja kwa moja, nje ya kuona picha ya kinachogombewa au kutafutwa kwa maana ya mpangilio wa changamoto na tamati au miundo ya suluhu, majawabu yanayotafutwa.

Kutaka upatikane mfumo ulioboreshwa wa kufunza walimu, inaashiria hakuna tatizo katika mitaala au haliwezi kutatuliwa kwa viwango vya ualimu vya sasa.

Ndiyo hapo kuna mchanganyiko wa changamoto inayohitaji kutatuliwa na msingi wa changamoto hiyo, hali inayoashiria kukwama katika 'kuidadavua' changamoto na kukabiliana nayo jinsi ilivyo, hivyo kuhamishia suala katika ngazi nyingine.

Kwa mfano, katika mitihani ya darasa la saba mwaka huu, idadi ya wanafunzi waliofaulu kwenda sekondari inakaribia asilimia 87.5 na ilikuwa ni nyongeza kwa ufaulu wa mwaka jana.

Siyo rahisi kwa wadau kukubaliana kuwa na mitaala itakayopunguza ufaulu wa wanafunzi, hivyo wanajaribu kuinua tu viwango.

Ina maana kwamba, mitaala kimsingi ubaki pale pale, na viwango vya ufaulu visiguswe au kuwako'bughudha' ya aina yoyote kwa suala hilo, ila wanafunzi waliofaulu wawe na viwango vikubwa zaidi vya uelewa kuliko ilivyo sasa, au ilivyo kawaida.

Ni mkanganyiko wa kimantiki ambao Waingereza huita 'squaring a circle' yaani upewe mduara halafu kazi yako ni kuubadili uwe mraba. Mitaala iliyopo na viwango vya ufaulu  vyote ni vizuri, lakini kuna tatizo kuwa wanafunzi wanamaliza darasa la saba hawajui kusoma na kuandika, wanamaliza shahada na huwezi kumpa insha fupi akaiweka tofauti kwa maneno yake mwenyewe.

Ni insha ya maneno 1,000 halafu inatakiwa ielezwe kwa maneno takriban 100 na isipoteze ladha au mtiririko wake. Sasa kijana aliyezoea 'multiple choice' na kukariri 'past papers' ataanzia wapi kufupisha insha?

Licha ya kuwa wataalamu wameketi kujadili jinsi ya kuboresha mitaala ya ufundishaji wa waalimu bado tatizo linabaki katika elimu inayotakiwa, na kwa maana hiyo viwango ambavyo inabidi vizingatiwe ili ithibitishwe kuwa elimu hiyo inajengeka.

Ni suala la kufaulu kwa msingi wa mtaala unaoleta matunda katika maeneo ambayo sasa yanaleta changamoto, ikiwa ni pamoja na ustadi wa kujieleza kwa kuchanganua dhana au mifumo ya fikra, na siyo mazungumzo ya kawaida.

Elimu ya kukariri inapwaya akipewa tatizo la kimazingira, kwani anapenda tu hesabu, wakati kinachotakiwa ni kuanza kupambanua mazingira tofauti yanahitaji hesabu gani, mtitiriko.

Kabla ya kukamiilisha mjadala wa mtaala unaohitajika ili kupata wahitimu wa aina hii au ile, yenye kuleta ladha au tija katika mazingira ya kiufundi (iwe ni ajira au changamoto nyingine), kuna tatizo la uelekeo wa kupungua kumudu lugha ya kufundishia.

Inawezekana kabisa mengi kati ya matatizo ya kudhihirisha elimu yanatokana na upana mdogo wa kuchangiana mawazo mwalimu anapokuwa na wanafunzi darasani, kwani anatembea katika lugha ya kufundishia kwa tahadhari na atakwepa kuongeza muda kubadilishana mawazo.

Pia kufundishia hakuwezi kubadilika katika mazingira ya kutaka ufaulu na kumridhisha kila mtu na hata kungekuwapo nafasi ya kutohangaikia kuridhisha watu, bado mtaala wa kufelisha wanafunzi utakuwa hauna mwenyewe.

Cha kufanya katika elimu ni kuongeza ufundishaji, ili kufikia kiwango kinachotaliwa kwa kila mwanafunzi, au kwa ngazi husika.

Ndiyo maana uwepo wa sekondari kwa kila mwanafunzi kimsingi ni kama uboreshaji wa shule za msingi, kwani wataalamu wanakiri wahitimu hawajui kusoma na kuandika.




Picha ya juu na chini ni Walimu tofauti wakiwa darasani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

HABARI KIMATAIFA

## Shilingi ya bahati yamponza ndani ya ndege

**BEIJING,** China

MWANAUME mmoja raia wa China ambaye ni mara yake ya kwanza kupanda ndege, ametozwa faini kwa kurusha sarafu ya kumtakia kheri katika injini ya ndege.

Mwanaume huyo mwenye umri wa miaka 28, alitakiwa kulipa dola 17,200, kama fidia ya kuingilia bajeti ya ndege hiyo inayoitwa 'Lucky Air'.

Ndege hiyo ilibidi itue baada ya kuona kuna sarafu ikiwa karibu na injini. Lu Chao, alikiri kurusha sarafu wakati akiwa anapanda ndege hiyo ambayo inasafiri ndani ya nchi, katika uwanja wa ndege wa Anqing Tianzhushan uliopo mashariki ya China.

Abiria huyo alishtakiwa Februari 2019, na alifikishwa mahakamani mwezi Julai na hukumu ilitangaza hivi karibuni. Ndege ilikatisha safari yake baada ya mfanyakazi mmoja alipoona sarafu karibu na injini ya ndege.

Wakati wanaangalia usalama, walitia gharama ya kuwatafutia abiria ndege nyingine ili waendelee na safari. Lu alishikiliwa katika kituo cha polisi kwa muda wa siku 10, na kushtakiwa kwa kuvuruga mpangilio uliokuwa umewekwa na hivyo alitakiwa kulipa fidia.

Mahakamani ndege hiyo ya Lucky Air ilisema kuwa iliwagharimu zaidi ya dola 17,600 kulipa nauli. Hata hivyo, Lu alidai kuwa ndege hiyo ilipaswa kutoa angalizo kwa abiria kuwa hairuhusiwi kurusha sarafu ndani ya ndege. **BBC**

## Ugiriki, Israel, Cyprus zalaani kupeleka wanajeshi Libya

**ATHENS,** Ugiriki

HATUA ya Uturuki kukubaliwa na bunge kuwapeleka wanajeshi wake nchini Libya, kunaongeza mvutano na mahasimu wake.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa na Ugiriki, Israel na Cyprus, imesema uamuzi huo ni ukiukaji mkubwa wa azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa linaloweka marufuku ya silaha nchini Libya na kuhujumu juhudi za jamii ya kimataifa za kutafuta suluhisho la amani na kisiasa nchini humo.

Bunge la Uturuki limeidhinisha kwa wingi mkubwa muswada huo ambao unaruhusu wanajeshi kupelekwa Libya.

Hatua hiyo inasafisha njia ya ushirikiano zaidi kati ya Uturuki na Libya lakini huenda wanajeshi hao wasipelekwe nchini humo haraka.

Bunge la Libya limeilaani hatua hiyo likiita uhaini wa hali ya juu.

Navyo vikosi vya Libya vya mashariki mwa nchi hiyo vimesema vimewataka raia kuchukua silaha na kupambana na wanajeshi wa Uturuki kama watapelekwa nchini humo kupigana. **DW**

# Marekani yamuua Jenerali Qasem Soleimani

**WASHINGTON,** Marekani

QASEM Soleimani, Jenerali wa vikosi vya Qudsi vinavyoungwa mkono na Iran, ameuawa na vikosi vya Marekani nchini Iraq.

Pentagon imethibitisha kuwa aliuawa kufuatia amri ya Rais Donald Trump.

Taarifa hiyo imetolewa kufuatia mashambulio katika Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Baghdad, ambako watu kadhaa wameuawa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Javad Zarif, ametaja hatua hiyo kuwa ni ya hatari na uchokozi.

Jenerali Soleimani alikuwa mtu mashuhuri kwa utawala wa Iran. Kikosi chake cha Qudsi kilikuwa kinaripoti moja kwa moja kwa kiongozi mkuu wa kidini wa Iran Ayatollah Ali Khamenei na alisifiwa kama shujaa wa kitaifa.

Rais Trump aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter na kuambatanisha picha ya bendera ya Marekani baada ya kutangazwa kuuawa kwa jenerali hiyo.

**Alikuwa kiungo muhimu katika mapambano ya kimkakati mashariki ya kati kupitia vikosi vya Kikurdi.**

Bei ya mafuta duniani imepanda kwa asilimia nne baada ya shambulio hilo.

"Kufuatia agizo la Rais, Jeshi la Marekani lilichukua hatua ya kuwalinda wafanyakazi wake nje ya nchi kwa kumuua Qasem Soleimani," taarifa ya Pentagon ilisema.

"Hatua hii ililenga kudhibiti mipango ya Iran ya mashambulio ya siku zijazo. Marekani itaendelea kuchukua hatua madhubuti kuwalinda watu wetu na maslahi yetu kote duniani."

Shambulio hili linakuja baada ya siku kadhaa za maandamano, ambapo waandamanaji walishambulia ubalozi wa Marekani mjini Baghdad na kukabiliana na vikosi vya Marekani katika eneo hilo.

Pentagon inasema Jenerali Soleimani aliidhinisha mashambulio dhidi ya ubalozi.

Maandamano yaliendelea nje ya ubalozi wa Marekani mjini Baghdad.

Kikosi maalum cha Jeshi la Iran, kimesema kiongozi wa waasi, Abu Mahdi al-Muhandis pia ameuawa katika shambulio hilo lililotekelezwa na Marekani. Hata hivyo ililaumu mashambulio ya helikopta ndani ya nchi hiyo.

Ripoti zinaashiria kuwa viongozi kadhaa wa waasi wa Iraq, wanazuiliwa na vikosi vya Marekani mjini Baghdad, japo taarifa hizo hazijathibitishwa.

Tangu mwaka 1998, Meja Jenerali Qasem Soleimani, ameongoza vikosi vya Kikurdi nchini Iran, kitengo maalum cha Jeshi la Iran ambacho huendesha opereshani zake nje ya nchi.

Alikuwa kiungo muhimu katika mapambano ya kimkakati mashariki ya kati kupitia vikosi vya Kikurdi.

Jina lake lilianza kuwa maarufu alipopewa nafasi ya kuongoza kikosi cha Quds na kujenga ushirikiano wa karibu na kiongozi mkuu wa kidini Ayatollah Khamenei. **BBC**



Jenerali Qasem Soleimani akiwa na maofisa wakati wa uhai wake, kiongozi hiyo wa jeshi aliuawa na ndege za kimarekani katika shambulio lililofanyika juzi mjini Baghdad. **PICHA: AFP**

# Iran yaapa kulipiza kisasi

**TEHRAN,** Iran

IRAN imeapa kulipiza kisasi kufuatia shambulizi la angani lililomuua jenerali wa ngazi ya juu wa nchi hiyo Qassem Soleimani.

Kuuawa kwa mkuu huyo wa Jeshi Maalum la Iran, kunaashiria kuongezeka kwa mgogoro kati ya nchi hizo mbili.

Mgogoro huo umekuwa ukitokota tangu Rais Donald Trump, alipojiondoa katika mkataba wa nyuklia wa Iran na kutangaza vikwazo vipya vinavyohujumu uchumi wa nchi hiyo.

Kiongozi wa juu kabisa wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei, ameonya kuwa watachukua hatua kali za kulipiza kisasi.

Ametangaza siku tatu za maombolezi kufuatia kifo hicho.

Waziri wa Mambo ya Nchi za Kigeni wa Iran, Mohammad Javad Zarif, amelaani mauaji hayo.

Jenerali Soleimani aliuawa pamoja na Abu Mahdi al-Muhandis, Naibu Kamanda wa Wanamgambo wa Iraq wa Popular Mobilization Forces (PMF).

Kundi hilo la PMF linaloungwa mkono na Iran, limepoteza watu wengine watano baada ya msafara wao kulengwa katika shambulizi la angani karibu na Uwanja wa Ndege wa Baghdad.

Wizara ya Ulinzi ya Marekani imesema ilimuua Soleimani kwa sababu alikuwa akipanga kuwashambulia wanadiplomasia na wanajeshi nchini Iraq na kote katika kanda hiyo. **DW**

# HADITHI


WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- 34

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**




**Ni hivi Kadili, kwa heshima yake, bila kuhofia chochote. Bila kumhofia mama yako, wala Eliza, nenda kamchukue mpeleke kwanza nyumbani akaonane na mama yako. Atie baraka kwenye nyumba yenu.**

"Majibu yenu yanafanana. Yeye kasema ni kweli alikuja hapa na mkaongea mambo mengi, lakini hamna uhusiano wowote ule."

"Alijibu sahihi."

"Mimi hilo halinipi tabu sana, ila nina mpango wa kumfanya Eliza awe na furaha."

"Ni kweli hana furaha, anataka uwe muwazi kwake, umchumbie kama wazazi wenu wanavyotaka au umuache awe huru."

"Ni kweli Meze. Kwa nilipofikia, napenda tu kukufahamisha kuwa uwezekano wa kumuoa Eliza ni mdogo sana."

"Kwa nini?"

"Naona niko karibu mno kumpata Edina." Alijibu Kadili na macho yake yaliyoonyesha kuwa ana uhakika na anachokisema.

"Umekutana naye wapi? Mumewe je, itakuwaje?"

"Kwa kifupi moja ya jambo lililonifanya nije hapa ni hili. Edina alikuja hapa majuzi kunitafuta, navuka barabara tu nikaitwa na mtoto mmoja hivi, kuna gari ilikuwa imepaki, kumbe yake, alifuata tu ramani ya Tandale akanipata. Alinichukua na kunipeleka kwenye hoteli ambayo amejificha kwa sasa. Amenihadithia vitu vingi, kumbe aliolewa kinguvu na matakwa na mama yake. Na aliambiwa akikataa basi mama yake ataniua mimi. Akakubali. Jamaa mwenyewe kumbe ana wanawake kibao. Edina alipogundua walikorofishana akamtoroka. Mama yake Mama Pauline ndipo alipopatwa na ugonjwa na moyo na kufariki.

Hakuna hata mmoja aliyemwambia mwenzake mambo ya mapenzi, lakini vitendo vyetu na maneno vinaelekea huko. Edina amehatarisha sana maisha yake kwa ajili yangu. Hii inaonyesha kabisa kuwa ananipenda." Kadili alijimwambafai.

"Ndugu yangu kama hayo unayosema ni kweli, basi ile ndoto yetu kwa Edina inaweza kuwa iko karibu kutimia." Meze aliongea akiwa na furaha.

"Sawa inawezekana kabisa ikawa hivyo, Eliza je?" Lilikuwa ni swali lisilotegemea kutoka kwa Kadili.

"Unamuuliza nani?" Meze naye aliuliza.

"Nakuuliza wewe." Alijibu Kadili na wote wakaangua kicheko.

******************************************

Ilitimu majira ya saa 10 jioni. Kadili na Meze bado walikuwa kwenye kijiwe chao wakizungumza mambo mbalimbali ya kifamilia na binafsi.

Mara mlio la meseji unaita kwenye siku ya Kadili. Aliingiza mkono mfukoni na kutoa simu yake ya tahadhari.

Kidole chake kimoja kilifanya kazi ya kufungua meseji hiyo na macho yake akaelekea kwenye kioo cha simu akaisoma.

Macho ya Meze yalikuwa yakimwangalia kwa makini Kadili. Alibaini tabasamu mwanana kwenye uso wake.

"Amekuja." Ilikuwa ni sauti laini ya Kadili kana kwamba anajiambia mwenyewe.

"Nani?"

"Edina yupo barabarani hapo amefika, anasema niende nikamchukue."

"Mhh 'kakusapraizi' mwanangu, leo laivu ndani ya nyumba ushindwe mwenyewe." Meze alimtania mwenzake.

"Nifanyeje, nimchukue nimpeleke nyumbani, au nimlete moja kwa moja hapa kijiweni?"

Kadili alimuuliza rafiki yake, kwani alionekana kachanganyikiwa kidogo kutokana na kutokuwa na maandalizi yoyote ya kumpekea mrembo Edina, mtoto wa kitajiri.

"Ni hivi Kadili, kwa heshima yake, bila kuhofia chochote. Bila kumhofia mama yako, wala Eliza, nenda kamchukue mpeleke kwanza nyumbani akaonane na mama yako. Atie baraka kwenye nyumba yenu.

Halafu baadaye anaweza kuja hapa ili tuongee naye mazungumzo yetu binafsi ambayo hayapaswi yasikike na mama pamoja na Eliza." Yalikuwa ni maneno ya Meze ambayo moja kwa moja Kadili aliyakubali.

"Ndiyo maana umeendelea kuwa rafiki yangu bora kabisa." Alisema Kadili huku akimkumbatia Meze.

"Twende tukamchukue." Kadili alimnong'oneza rafiki yake.

***********************************

Mlango wa gari ulifunguka. Edina aliteremka ndani ya gari kwa madaha. Baadhi ya akinadada na akinamama waliokuwa wakipita hapo walishindwa kuendelea na safari zao kwa kumtazama.

Alionekana ni tofauti kabisa nao. Nadhani walikuwa wakijiuliza, msichana mzuri na mrembo kama huyo ametokea wapi.

Ni kama maajabu ya kumuona twiga akiwa mjini badala ya mbugani.

Dar es Salaam ikiwa imefurika wasichana warembo kupindukia, wengi wao wakiwa wameuongeza urembo wao wa asili maradufu kwa vipodozi lukuki vilivyofurika madukani, lakini si kwa msichana huyu Edina.

Uzuri wake ulikuwa ni asili, akiongeza na urembo wa kike ambao haujamfanya kubadilika kupota kiasi au kuchusha.

Ngozi yake maji ya kunde iliifanya imeremete na kushawishi kuigusa. Tabasamu lake la pia ni jambo la kawaida katika uso wake. ambalo lingeweza kununuliwa kwa fedha tu iwapo mwenyewe angejali kujiunga na chuo kimojawapo cha usanii na kuhitimu. Hali kadhalika, ziada hii haikutokana na macho yake maangavu, pua yake iliyochongoka wala meno yake meupe yaliyojipanga kikamilifu kinywani mwake kama mistari miwili ya punje za mahindi kwenye kibunzi.

Wanaume na vijana waliokuwepo eneo hilo nao hawakuwa nyuma kwenye mshangao kwa malkia huyo alishuka ndani ya gari alilokuwa akiendesha mwenyewe.

Umbile la msichana huyo liliwafanya kuwa kama wamepigwa ganzi. Siku hiyo hakuweka dawa ya aina yoyote ile kwenye nywele na kuzidi kuzipa mvuto.

Siku hiyo alivaa mavazi yenye heshima, sketi ndefu iliyovuka magoti na blauzi nyepesi iliyokifanya kifua chake kitoe picha ya uhai wa matiti yake.

Nadhani alijua anakokwenda. Moja kwa moja alikwenda kumkumbatia Meze.

"Shemeji, habari za siku nyingi?" Yalikuwa ni maneno machache, lakini yakagonga kwenye vichwa vya wote wawili, Kadili na Meze.

Meze alijua kabisa maana na neno shemeji. Alitambua sasa Edina ameweka wazi nia yake ya kuwa na Kadili, maana si kwa kumwita shemeji hivi hivi tu.

Mshtuko ulimpata pia Kadili. Pamoja na kwamba dalili zote zinaonyesha kuwa Edina anaelekea kuwa mpenzi wake, lakini hakuna sehemu yoyote ambayo wametamkiana kuwa wanapendana kimapenzi.

Lakini neno 'shemeji' alilolitamka kwa Meze, linaashilia, huo ni mwisho ya yale yote ambayo alikuwa akiota, akiomba.

"Nadhani hakuna kipingamizi tena, leo hii nitamwambia kuwa napenda na yeye atasema kilicho moyoni mwake, natumaini kuwa anasema ananipenda kwa sababu vitendo vyake vinaonyesha hivyo." Aliwaza Kadili.

Alimwita kijana mmoja na kumkabidhi noti ya sh 1,000 ikiwa pamoja na kumpa maelekezo ya kulinda gari iliyopaki hapo hadi watakaporejea.

"Mbona hujaniambia kuwa unakuja mama?" Kadili alianza kwa kumlaumu, kabla ya kufuatiwa kicheko chepesi kutoka kwa Edina.

"Nilitaka 'kukusapraizi', sikutaka kukwambia na kukusumbua kufanya maandalizi yasiyo ya lazima, au nimekosea baba."

"Hapana, maana nilitaka kukuchinjia kuku." Alijibu na wote watatu wakaangua kicheko.

Wakati huo, tayari walikuwa wanaongozana kwenda nyumbani kwa kina Kadili.

Edina alikuwa kati. Upande wake wa kushoto alikuwa Kadili na walikuwa wameshikana mikono.

Upande wake wa kulia alikuwa Meze. Mkono wa Edina ulikuwa begani kwake, hivyo kuleta picha nzuri, iliyowavutia wengi waliowaona na kupishana nao, lakini bila kujua pale mwenye mali ni nani, hali iliyowafanya wambea washindwe kubaini.

**Itaendelea Jumamosi**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA /MASHAMBA

**Viwanja vinauzwa** Kibaha Misugusugu. Ukubwa ni mita 20 kwa 20 (400m2). Bei ni 2,000,000/- Milioni mbili tuu. (5,000/=1m2). Unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mine. Huduma zote zipo. Kwa mawasiliano: 0714 090009 / 0767 090008. Vimepimwa.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0782253676**


### CHETI KIMEPOTEA



115573002

**TUMAINI AGABU MGOGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.3437/0048** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2010 katika shule ya Sekondari KYIMO. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **TUK/RB/1622/17.**

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NASSORO MTORO SHAWEJI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 264 AZT** aina ya **T.B 150.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/GOG/RB/599630/2019.**

115573102

### PROSHARE CAPITAL LTD

Kutangaza magari yanayouzwa;

**EMMANUEL E. KASEMBE**
- (TOYOTA DUET *T 610 CEE)*

**NTULI K. MWAMUKONDA**
- NISSAN PATROL *T 664 BSC*

115572702

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**YOHANA JOHN MSIGALA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 196 BXV** rangi Nyeusi. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/60503/2019.**

115573602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**MCA/84**

**Mahakama ya Mwanzo ya KAWE**
**Wilaya ya KINONDONI**

**MADAI NAMBARI 114 YA 2019**

**Mdai:.......................................FRANK FESTO KISSIMA**

**Amdai**

**Mdaiwa: ......BANJI CARGO HAULIERS (NAZIM BHANJI)**

**Kwa: BANJI CARGO HAULIERS (NAZIM BHANJI) P.O. Box 105593, DSM.**

Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta/madai yake/yao kwamba/Eleza hapa habari ya madai **KUJIBU DAI LAKO LA PESA 13,000,000/- NA ZAIDI**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya.........tarehe **17/01/2020 saa 2.30 asubuhi/** Alasiri kwa kujibu madai haya. Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wake/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa hati hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo tarehe 3/1/2020.

..........................................
Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo
MAHAKAMA YA MWANZO
KAWE

115573302

### CHETI KIMEPOTEA



115572902

**AINA HAMIS KIPENDAROHO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1343.0003** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa Mwaka 2011 katika shule ya Sekondari ANNE MARIE. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/5473/2020.**


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Alisson ashinda tuzo ya Samba d'Or Brazil

**SAO PAULO,** Brazil

ALISSON amekuwa golikipa wa kwanza kushinda tuzo ya Samba d'Or nchini Brazil, akimpiku mchezaji mwenzake wa Liverpool, Roberto Firmino, huku Neymar akishika nafasi ya tano.


Kipa huyo alipata asilimia 35.54 ya kura zote kwa tuzo hiyo inayotolewa kwa mchezaji wa Brazil anayecheza Ulaya, huku Firmino akishika nafasi ya pili kwa kupata asilimia 23.48 ya kura zote.

Liverpool ilishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super na Klabu Bingwa ya Dunia mwaka jana, huku Brazil ikishinda taji la Copa America (michuano ya mataifa ya Amerika Kusini).

Beki wa Paris Saint-Germain, Thiago Silva alishika nafasi ya tatu, huku kiungo wa Liverpool, Fabinho, akishika nafasi ya nne.

Mshindi mara tatu wa tuzo hiyo, Neymar, ambaye alikosa kuichezea Brazil wakati ikitwaa taji la Copa America kwenye ardhi ya nyumbani, alimaliza nafasi ya tano kwa kupata asilimia 7.57 ya kura zote.

Firmino alishinda tuzo hiyo mwaka 2018 na Philippe Coutinho mwaka 2016.





# KLOPP ATHIBITISHA KEITA KUIKOSA EVERTON

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amethibitisha kuwa, Naby Keita ataukosa mchezo wa Kombe la FA dhidi ya wapinzani wao wa Merseyside, Everton utakaochezwa kesho Jumapili baada ya kuumia nyonga katika mchezo wa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Sheffield United.

Awali Keita alitajwa kuwa kwenye kikosi cha kwanza kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu, lakini alijitonesha kwenye mazoezi na hivyo kuwakosa Sheffield na nafasi yake akapewa James Milner katika kiungo ya kati.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Guinea mwenye umri wa miaka 24 amekuwa na matatizo ya majeruhi mara kwa mara tangu alipotua hapo akitokea RB Leipzig, na amecheza mechi 24 tu kwenye Ligi Kuu tangu kuwasili kwake.

Na sasa anaonekana atakuwa tena nje ya dimba kwa muda, ingawa Klopp hakutaja ni muda gani mchezaji huyo atakaa nje.

"Kwa uhakika kabisa sijui, lakini ilikuwa ni nyonga, lakini tayari naweza kusema kuwa hatakuwapo katika mchezo dhidi ya Everton," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Hiyo inatufanya tuwe na wachezaji wakubwa 12 pamoja na wale chipukizi, ndio hivyo na hatuwezi kubadili lolote.

"Sijui namna gani ilitokea, nafikiri alipojaribu kupiga mpira kwenye mazoezi ya kujiandaa na mchezo. Alikuwa kwenye vyumba vya kubadilishia nguo akiwa anachechemea.

"Kila mmoja aliyewahi kucheza mpira anajua aina hii ya majeruhi sio nzuri, inaumiza. Sijui kwa uhakika kabisa atakaa nje kwa muda gani, lakini ninachoweza kusema hatakuwapo kwenye mchezo wa Jumapili."

Baada ya mchezo huo wa Jumapili, Liverpool mchezo wake unaofuata wa Ligi Kuu ni dhidi ya Tottenham utakaopigwa Januari 11 mwaka huu.

# Juventus yakamilisha usajili wa Dejan Kulusevski

**TURIN,** Italia

JUVENTUS imekamilisha usajili wa Dejan Kulusevski kutoka Atalanta kwa ada ya awali ya euro milioni 35 na ameruhusiwa kubakia kule Parma kwa mkopo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Sweden, Kulusevski amesaini mkataba wa miaka minne na nusu na ada yake inaweza kuongezeka kwa euro milioni 9 kama bonasi.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 19 alijiunga tena na Atalanta akitokea Brommapojkarna mwaka 2016 na amecheza mechi tatu katika kikosi cha kwanza kabla ya kupelekwa kwa mkopo Parma kwa msimu wa 2019-20.

Kulusevski amekuwa na wakati wa kuvutia kwenye uwanja wa Ennio Tardini, akifunga mabao manne na kutoa 'asisti' saba katika mechi 17 alizocheza kwenye ligi, na atabakia kule hadi mwishoni mwa msimu kwa mujibu wa makubaliano na Juve.

Ujio wa Kulusevski unaweza kutoa mwanya wa Emre Can kuondoka kwa Bianconeri hao mwishoni mwa msimu na hataondoka Januari kama ilivyoripotiwa awali.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, Can amecheza mechi saba tu kwa Juve msimu huu na amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu za Paris Saint-Germain, Manchester United na Borussia Dortmund.



HABARI MICHEZO

# Alisson ashinda tuzo ya Samba d'Or Brazil

**SAO PAULO,** Brazil

ALISSON amekuwa golikipa wa kwanza kushinda tuzo ya Samba d'Or nchini Brazil, akimpiku mchezaji mwenzake wa Liverpool, Roberto Firmino, huku Neymar akishika nafasi ya tano.


Kipa huyo alipata asilimia 35.54 ya kura zote kwa tuzo hiyo inayotolewa kwa mchezaji wa Brazil anayecheza Ulaya, huku Firmino akishika nafasi ya pili kwa kupata asilimia 23.48 ya kura zote.

Liverpool ilishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super na Klabu Bingwa ya Dunia mwaka jana, huku Brazil ikishinda taji la Copa America (michuano ya mataifa ya Amerika Kusini).

Beki wa Paris Saint-Germain, Thiago Silva alishika nafasi ya tatu, huku kiungo wa Liverpool, Fabinho, akishika nafasi ya nne.

Mshindi mara tatu wa tuzo hiyo, Neymar, ambaye alikosa kuichezea Brazil wakati ikitwaa taji la Copa America kwenye ardhi ya nyumbani, alimaliza nafasi ya tano kwa kupata asilimia 7.57 ya kura zote.

Firmino alishinda tuzo hiyo mwaka 2018 na Philippe Coutinho mwaka 2016.





# KLOPP ATHIBITISHA KEITA KUIKOSA EVERTON

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amethibitisha kuwa, Naby Keita ataukosa mchezo wa Kombe la FA dhidi ya wapinzani wao wa Merseyside, Everton utakaochezwa kesho Jumapili baada ya kuumia nyonga katika mchezo wa ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Sheffield United.

Awali Keita alitajwa kuwa kwenye kikosi cha kwanza kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu, lakini alijitonesha kwenye mazoezi na hivyo kuwakosa Sheffield na nafasi yake akapewa James Milner katika kiungo ya kati.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Guinea mwenye umri wa miaka 24 amekuwa na matatizo ya majeruhi mara kwa mara tangu alipotua hapo akitokea RB Leipzig, na amecheza mechi 24 tu kwenye Ligi Kuu tangu kuwasili kwake.

Na sasa anaonekana atakuwa tena nje ya dimba kwa muda, ingawa Klopp hakutaja ni muda gani mchezaji huyo atakaa nje.

"Kwa uhakika kabisa sijui, lakini ilikuwa ni nyonga, lakini tayari naweza kusema kuwa hatakuwapo katika mchezo dhidi ya Everton," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Hiyo inatufanya tuwe na wachezaji wakubwa 12 pamoja na wale chipukizi, ndio hivyo na hatuwezi kubadili lolote.

"Sijui namna gani ilitokea, nafikiri alipojaribu kupiga mpira kwenye mazoezi ya kujiandaa na mchezo. Alikuwa kwenye vyumba vya kubadilishia nguo akiwa anachechemea.

"Kila mmoja aliyewahi kucheza mpira anajua aina hii ya majeruhi sio nzuri, inaumiza. Sijui kwa uhakika kabisa atakaa nje kwa muda gani, lakini ninachoweza kusema hatakuwapo kwenye mchezo wa Jumapili."

Baada ya mchezo huo wa Jumapili, Liverpool mchezo wake unaofuata wa Ligi Kuu ni dhidi ya Tottenham utakaopigwa Januari 11 mwaka huu.

# *Juventus yakamilisha usajili wa Dejan Kulusevski*

**TURIN,** Italia

JUVENTUS imekamilisha usajili wa Dejan Kulusevski kutoka Atalanta kwa ada ya awali ya euro milioni 35 na ameruhusiwa kubakia kule Parma kwa mkopo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Sweden, Kulusevski amesaini mkataba wa miaka minne na nusu na ada yake inaweza kuongezeka kwa euro milioni 9 kama bonasi.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 19 alijiunga tena na Atalanta akitokea Brommapojkarna mwaka 2016 na amecheza mechi tatu katika kikosi cha kwanza kabla ya kupelekwa kwa mkopo Parma kwa msimu wa 2019-20.

Kulusevski amekuwa na wakati wa kuvutia kwenye uwanja wa Ennio Tardini, akifunga mabao manne na kutoa 'asisti' saba katika mechi 17 alizocheza kwenye ligi, na atabakia kule hadi mwishoni mwa msimu kwa mujibu wa makubaliano na Juve.

Ujio wa Kulusevski unaweza kutoa mwanya wa Emre Can kuondoka kwa Bianconeri hao mwishoni mwa msimu na hataondoka Januari kama ilivyoripotiwa awali.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, Can amecheza mechi saba tu kwa Juve msimu huu na amekuwa akihusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu za Paris Saint-Germain, Manchester United na Borussia Dortmund.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UNITED YAJIPANGA KUMSAJILI MADDISON

## Lengo ni kuona safu yake ya kiungo inaimarika huku hatima ya Pogba...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imejipanga kuimarisha safu yake ya kiungo katika kipindi cha dirisha dogo la usajili la Januari kwa kumsajili James Maddison na Jack Grealish.

**United imewataja nyota hao wawili kuwa ni wachezaji inaotaka kuwapa mikataba ya kutua Old Trafford mwezi huu.**

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer, anahitaji kuongeza nguvu kwenye idara yake ya kiungo, huku pia akimtaja, Scott McTominay kwenye mawindo na Paul Pogba akiendelea kuuguza maumivu ya enka yanayomsumbua.

Gazeti la The Independent, limeandika kuwa nyota wa Leicester, Maddison na Grealish wa Aston Villa, ni wachezaji wanaotakiwa kutua klabuni hapo ili kuimarisha kikosi cha United, wakati kiungo Christian Eriksen naye pia akiwa kwenye mawindo, lakini nyota huyo wa Tottenham anaonekana kama anajiandaa kwenda kucheza soka nje ya England.

Maddison amekuwa katika kiwango bora na kuisaidia Leicester kufanya vizuri msimu huu, nyota huyo amefunga mabao tisa na kutengeneza nafasi tatu za kufunga katika mechi za mashindano yote.

Wakati kwa upande wa Grealish, yeye amezifumania nyavu mara nane na amewatengenezea wachezaji wenzake nafasi nyingine sita za kufunga.

United inajipanga kujiimarisha baada ya kuanza vibaya msimu huu na kwa sasa iko katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Kikosi hicho cha Solskjaer kilikosa ubunifu na bahati katika mchezo dhidi ya Arsenal iliyochezwa Jumatano iliyopita na kumalizika kwa kukubali kichapo cha mabao 2-0, huku Jesse Lingard akipangwa kucheza katika nafasi ya kiungo mshambuliaji mbele ya Fred na Nemanja Matic.

United ililazimika kuwaingiza Andreas Pereira na Juan Mata, ambao walianzia benchi katika mechi hiyo dhidi ya Arsenal, lakini ni wazi kuwa klabu hiyo inahitaji kusajili wachezaji wenye viwango vizuri kwenye safu hiyo ya kiungo.

## ZISIKUPITE

### UNITED KUMUUZA POGBA

MAISHA ya Paul Pogba katika kikosi cha Manchester United yamefikia mwisho baada ya uongozi wa klabu hiyo kuamua kumuuza. Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26, anaweza kutua Real Madrid, huku pia kukiwa na tetesi za Toni Kroos (29), kutua Old Trafford. ***(Sun)***

### CAN, LONGSTAFF SOKONI

KIUNGO wa Juventus na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Emre Can (25), na kiungo wa Newcastle, Sean Longstaff, ambaye ana umri wa miaka 22, pia wametajwa kutakiwa na Manchester United. ***(ESPN)***

### CANTWELL AGOMBEWA

MANCHESTER United inajiandaa kuingia kwenye mbio za kuwania saini ya kiungo mchezeshaji wa Norwich, Todd Cantwell (21), ambaye anawindwa na Manchester City na Tottenham. Thamani ya nyota huyo imetajwa kuwa ni pauni milioni 30. ***(Mail)***

### ARSENAL, SPURS VITANI

ARSENAL na Tottenham zote zimeonyesha nia ya kumsajili winga wa Atletico Madrid, Thomas Lemar, ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Foot Mercato via Mirror)***

### GABIGOL AKARIBIA WEST HAM

WEST Ham inajipanga kumsajili straika Gabigol (23), kutoka Inter Milan baada ya kuonyesha kiwango kizuri alipokuwa kwa mkopo Flamengo. Thamani ya Mbrazil huyo imetajwa kuwa ni pauni milioni 20. ***(Sun)***

### BATSHUAYI ATAJWA VILLA

ASTON Villa inajipanga kumsajili wa mkopo straika wa Ubelgiji na Chelsea, Michy Batshuayi (26), lakini baadaye ikijiandaa kumpa mkataba wa kudumu endapo itafanikiwa kumpata. ***(Footmercato - in French)***

### GIROUD AKARIBIA VILLA

MABOSI wa Aston Villa wameweka wazi malengo yao wa kuwania saini ya mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Olivier Giroud, ambaye ana umri wa miaka 33. ***(Sun)***

### DEMIRAL KUIKAMUA ARSENAL

ARSENAL inaongoza katika vita ya kuwania saini ya beki wa kati wa Juventus, Merih Demiral (21). The Gunners inaamini kuwa ofa yao ya pauni milioni 42.5 itakubaliwa na kuwashinda Manchester United, AC Milan, Atletico Madrid na Schalke ambazo zinamwania pia beki huyo. ***(Fotomac via Sun)***

### ARTETA AMTAKA AKE

ARSENAL imeingia kwenye vita ya kuwania saini ya beki wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Nathan Ake, ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Telegraph)***

### FERNANDINHO MAMBO SAFI

MANCHESTER City inatarajia kumpa ofa ya mkataba mpya wa mwaka mmoja kiungo wake Mbrazil, Fernandinho, ambaye ana umri wa miaka 34. ***(Sun)***

### AJAX YACHEMKA KWA JAN

AJAX imeamua kusitisha mchakato wa kuwania saini ya beki wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Jan Vertonghen (32), kwa sababu thamani ya mchezaji huyo ni kubwa. ***(De Telegraaf - in Dutch)***

HABARI MICHEZO

# Mtibwa Sugar yatamani ubingwa

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, amesema kuwa kikosi chake hakijakata tamaa ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao unashikiliwa na Simba ya jijini Dar es Salaam.

Katwila (pichani chini) aliliambia gazeti hili kuwa idadi ya mechi zilizobakia za ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni nyingi, hivyo lolote linaweza kutokea katika msimamo.

Kocha huyo alisema kuwa bado timu yake haijacheza mechi dhidi ya vigogo, Simba na Yanga, na baada ya mechi hizo, ndiyo atajua mwelekeo wa timu yake katika mbio za kuwania taji hilo.

"Bado tuna nafasi ya kutwaa ubingwa, ngoma bado ni ngumu katika ligi hii, tunaweza kwenda hadi mechi ya mwisho ndio tutajua bingwa mpya," alisema kocha huyo ambaye alishinda taji la Afrika Mashariki na Kati kwa vijana wa umri chini ya miaka 20 (U-20).

Baada ya mechi yake ya jana ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mbao FC, iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Gairo, kikosi hicho kitasafiri kwenda Zanzibar katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi na itaanza kampeni ya kuwania taji hilo kwa kuwavaa Chipukizi hapo keshokutwa.

Timu nyingine za Bara zinazoshiriki michuano hiyo ni mabingwa watetezi, Azam FC, ambao watafungua dimba dhidi ya Mlandege wakati Simba itacheza dhidi ya Zimamoto huku Yanga wakiwakabili Mlandege.



# NIYONZIMA ATAMBA YANGA KUIBUKA NA USHINDI MNONO

**Na Somoe Ng'itu**

KIUNGO wa kimataifa wa Yanga, Haruna Niyonzima, amewataka mashabiki na wanachama wa timu hiyo, kujitokeza kwa wingi katika mechi dhidi ya watani zao itakayochezwa leo kwa sababu wachezaji wamejiandaa kuwapa furaha.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Niyonzima, amesema kuwa kikosi hicho kimejiandaa na kinajua thamani ya kupata ushindi katika mechi hiyo inayosubiriwa na mashabiki wengi wa soka nchini.**

Niyonzima alisema kuwa licha ya mechi hiyo kuwa ngumu, anawataka wachezaji wenzake kuongeza utulivu na umakini kila watakapokuwa na mpira.

"Nawaomba Yanga waje uwanjani, wasiwe na wasiwasi kuelekea mechi hii, ni mechi ngumu, lakini kwa wachezaji ambao tumecheza mechi hizi nyingi, tunajua wapi tunaweza kufaulu, wachezaji tunajuana vema, naamini tukifuata maelekezo ya makocha, hakuna kitakachoharibika," Niyonzima alisema.

Kiungo huyo wa zamani wa APR ya Rwanda alisema kuwa wachezaji wa Yanga wanahitaji kuona mashabiki wao wakiwa na furaha na kwa kufahamu hilo, wamejipanga kupambana katika mchezo huo.

"Tuko vizuri, tusiangalie mambo mengine ya nje ya uwanja, wachezaji wote tunajua thamani ya kushinda mechi ya watani, tunajua wanachohitaji mashabiki na wanachama wa Yanga, kikubwa tuombe uzima," alisema Niyonzima.

Aliongeza kuwa atafurahi kupata nafasi ya kucheza hapo kesho ili aisaidie timu yake kupata ushindi.

"Nilikuwa na nafasi mazoezi kila siku, niko vizuri, uamuzi wa kucheza uko chini ya mwalimu, narudia kusema kuwa mechi hii ninaiheshimu, ni mechi pia inayoweka rekodi na historia kwa kila mchezaji," Niyonzima alisema.

Niyonzima ambaye aliachwa na Simba alitua nchini juzi na kujiunga kwa mara ya pili na Yanga akitokea AS Kigali, inayoshiriki Ligi Kuu Rwanda.



Kocha Mkuu wa Simba, Sven VandenBroeck (kushoto), akimkabidhi jezi ya timu hiyo, winga mpya Luis Misquissone, kutoka UD Songo ya Msumbiji. Winga huyo aliwasili nchini juzi usiku na jana alikamilisha mazungumzo ya kujiunga na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara. **PICHA: SIMBA**

# Azam yatangulia mapema Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Azam FC kinaondoka jijini Dar es Salaam leo na kuelekea Zanzibar kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia kesho Visiwani humo.

Azam FC ambayo sasa inanolewa na Aristica Cioaba ndio mabingwa watetezi wa michuano hiyo ambayo mwaka huu inachezwa kwa mtindo wa mtoano.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Jaffer Iddi, alisema kuwa uamuzi wa kwenda mapema katika michuano hiyo unalenga kuwapa mapumziko wachezaji wao ambao wametoka kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Iddi alisema kuwa wanatarajia kwenda kupambana na hatimaye kufanya vema katika michuano hiyo inayofanyika kila mwaka.

Kiongozi huyo alisema kuwa ushindani walioupata katika mechi yao dhidi ya Singida United, umesaidia kuwaimarisha katika Ligi Kuu Bara na kuelekea kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi.

"Tumesharejea jijini Dar es Salaam tukitokea Arusha, na kesho (leo) Jumapili, tunatarajia kuanza safari ya kwenda Zanzibar, lakini ushindi tulioupata jana (juzi), dhidi ya Singida United umetusaidia kutuweka katika nafasi nzuri katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, tumerejea kwenye nafasi ya pili, nafasi ambayo kila mmoja anaitamani," alisema Iddi.

Hata hivyo kiongozi huyo alisema kuwa mchezo huyo ulikuwa mgumu, lakini uwezo wa wachezaji wao, ndio umesaidia kupata matokeo mazuri.

"Mchezo ulikuwa mgumu na wenye ushindani, tunamshukuru Mungu tumepata ushindi, na ushindi huo umetupa nguvu zaidi, tunahitaji kwenda mbele zaidi," alisema Iddi.

Katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Azam FC iko katika Kundi A na itaanza kutetea taji hilo kwa kucheza dhidi ya Mlandege hapo keshokutwa wakati mechi ya mapema itakuwa ni kati ya Mtibwa Sugar dhidi ya Chipukizi wakati Simba itawavaa Zimamoto na Yanga itaanza dhidi ya Mlandege siku ya Jumanne.

# Michezo

Jumamosi Januari 4, 2020

Nipashe





United yajipanga kumsajili Maddison

HABARI UK.30



KAGERE

SIBOMANA

## Azam yapania kurejea vitani

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuifunga Singida United mabao 2-1 na kupaa hadi nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, mshambuliaji wa Azam FC, Obrey Chirwa, amesema kikosi chao kimerejea kwenye ushindani.

Azam FC sasa ina pointi 26 baada ya kucheza mechi tatu ikiwa nyuma ya mabingwa watetezi Simba wenye pointi 34, huku Yanga ambayo imecheza mechi pungufu inafuatia ikiwa na pointi 24.

Akizungumza na gazeti hili jana, Chirwa, alisema kuwa kikosi chao kimerudi kwenye mbio za kuwania ubingwa na wamejipanga kuendelea kupambana ili kubakia katika nafasi hiyo ya pili katika msimamo wa ligi.

"Ligi ina ushindani mkubwa, hali hii itatufanya tupambane zaidi kusaka matokeo chanya, tutaendelea kufanya hivyo katika mechi zote zinazofuata," alisema Chirwa.

Mshambuliaji huyo alisema kuwa licha ya kuwa na changamoto wanapokwenda kwenye viwanja vya mikoani, bado wanaahidi kusaka matokeo mazuri ili watimize malengo yao ya kukata tiketi ya kushiriki katika mashindano ya kimataifa hapo mwakani.

# AMA ZAO AMA ZETU

## Sven, Mkwasa kila mmoja atamba kikosi chake kimejipanga kuondoka na ushindi katika mtanange huo...

**Na Somoe Ng'itu**

TAMBO na majigambo yaliyokuwa yanatawala kutoka kila kona ya mashabiki na wanachama wa klabu kongwe nchini, Simba na Yanga yanatarajiwa kumalizika baada ya vigogo hao kukutana katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Mechi hiyo ambayo itachezeshwa na "mwanadada", Jonesia Rukyaa, kutoka Bukoba mkoani Kagera, ni ya kwanza kwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2019/20, na pia ni ya kwanza kwa mwaka huu mpya wa 2020.**

Simba ambao ndio vinara wa Ligi Kuu Bara watashuka uwanjani leo wakiwa na rekodi ya ushindi wa mechi tatu mfululizo za ligi hiyo dhidi ya Lipuli FC, KMC FC na Ndanda FC, wakati Yanga ilitoka sare ya bila kufungana ugenini dhidi ya Mbeya City na imeshinda michezo miwili dhidi ya Tanzania Prisons na Biashara United.

Wekundu wa Msimbazi ambao wamecheza mechi 13, wana pointi 34 wakati Yanga ambayo imecheza mechi mbili pungufu iko katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi hiyo yenye kushirikisha timu 20 ikiwa imejikusanyia pointi 24.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara watashuka uwanjani pia wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0, walilopata katika mchezo wa marudiano walioupata msimu uliopita.

Akizungumza jijini jana, kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, Sven Vandenbroeck, alisema kuwa kikosi chake kiko tayari na imara kwa ajili ya mchezo huo na anaamini watapata matokeo mazuri.

Sven alisema kuwa anajua mechi ya watani wa jadi huwa na matarajio makubwa kwa kila upande, lakini kwake amekiweka vema kikosi chake ili kutimiza malengo waliyonayo ya kuwania ubingwa.

"Ni mechi ambayo pia inatoa taswira ya mbio za kuwania ubingwa, kikosi changu kiko imara, wachezaji wote wamefanya mazoezi vizuri isipokuwa Miraji (Athumani) na Rashid Juma, waliobaki wote wako tayari kwa mchezo wa kesho (leo)," alisema kocha huyo ambaye ataiongoza kwa mara ya kwanza Simba dhidi ya Yanga.

Naye nahodha wa Simba, John Bocco, alisema kuwa wanatarajia kupata ushindi katika mchezo huo kwa sababu kikosi cha timu yao kinaundwa na wachezaji wenye uzoefu na mechi 'kubwa' na zenye ushindani.

"Tuna muunganiko mzuri ndani ya uwanja na nje ya uwanja, sina mashaka kabisa na mchezo wa kesho, tunawaomba mashabiki wetu waendelee kuwa na imani na sisi, kikubwa tutaenda kupambana kwa ajili ya timu yetu ili tuweze kupata pointi tatu muhimu," alisema nahodha huyo.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Azam FC, alisema kuwa watashuka uwanjani kupambana kwa ajili ya kuweka heshima ya timu na wao wachezaji.

Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, alisema mechi ya leo ni ya kawaida kama ilivyo michezo mingine ya kawaida, lakini inatofautishwa na klabu zake kuwa na mashabiki wake. Mkwasa alisema kuwa malengo yao ni kupata ushindi katika mchezo huo na kikosi chake kina rekodi nzuri katika mechi zake mbili zilizopita.

Alisema kuwa kikosi chake kimejiandaa kupambana kupata ushindi na ameweka wazi kwamba mechi ya leo haitakuwa nyepesi kama wapinzani wanavyofikiria.

"Mechi mbili za mwisho, tumecheza na timu ambayo haijafungwa, sisi ndio tumefungua 'duka', wasifikirie Yanga ni timu nyepesi, na timu rahisi, mechi za Simba na Yanga, sio ngeni kwangu mimi, nimeweza kuwafunga nikiwa mchezaji, wamenifunga nikiwa mchezaji na kocha," alisema Mkwasa.

Aliwataja wachezaji ambao watakosa mechi ya leo ni beki, Lamine Moro, mwenye kadi tatu za njano, pamoja na mshambuliaji Tariq Seif, ambaye ni majeruhi.

"Tumetoka kwenye ratiba ngumu, tumesafiri umbali mrefu, tunaiheshimu mechi hiyo, tumepata matokeo mazuri katika mechi mbili ngumu zilizopita, tunataka kuendeleza ushindi kwa kuwafunga Simba na kusisitiza rekodi yao ya kucheza michezo mingi bila ya kufungwa," Mkwasa alisema.

Baada ya mechi ya leo, vigogo hao watasafiri kuelekea Zanzibar katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia keshokutwa visiwani humo kwa kushirikisha timu za hapa nchini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >